**Tiketi** za elektroniki mabasi zaleta mkanganyiko

UKURASA 7



**RC aagiza** DED, Ofisa Ardhi wawekwe selo

UKURASA 8

Jumatano Januari 6, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580452

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



**Inter wawania kumsajili Origi**

UKURASA 20

# NSSF yashtukia maofisa wake kuhujumu mafao



- **Mmoja** anaswa tuhuma za kupewa rushwa na mwajiri... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MBOWE ATAJA ILIKO HATIMA KINA MDEE KUFUTWA CHADEMA**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman...

UKURASA WA 3

**WIZARA YAMWEKA MTEGONI HAJI MANARA**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imemtega Msemaji Mkuu wa...

## Msako dawa za kuongeza nguvu kiume warindima

UKURASA 16



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akibonyeza kitufe kupiga king'ora kuashiria uzinduzi wa meli ya MV. Mbeya II kwenye Bandari ya Mbamba Bay wilayani Nyasa. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

# Mtoto wa miaka 11 adaiwa kujinyonga akitumia sweta

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA: NI USHINDI TU LEO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# NSSF yashtukia maofisa wake kuhujumu mafao

**Na Waandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limewaonya baadhi ya waajiri wanaoshirikiana na wafanyakazi wa shirika hilo kufanya hujuma ikiwamo kutoa rushwa ili kukwepa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alitoa onyo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

"NSSF tunakemea vitendo vya rushwa, ninapenda kusisitiza wanachama na wadau wanapoona kama kuna dalili zozote wanapokuwa wanataka huduma katika ofisi zetu nchi mzima wasisite kuwasiliana na uongozi wa NSSF kwa kuwasiliana moja kwa moja na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma au Mkurugenzi wa Uendeshaji au Mkurugenzi Mkuu au kutoa taarifa hizo kwenye vyombo vya dola," alisema.

Lulu alisema kuna baadhi ya waajiri wanashirikiana na baadhi ya wafanya kazi wa shirika hilo ambao wamekosa uadilifu na kuingia katika vitendo vya rushwa, jambo ambalo haliwezi kuvumiliwa na shirika.

Alisisitiza kuwa, NSSF imeendelea kudhibiti mianya ya rushwa na hivi karibuni katika ofisi ya NSSF Mkoa wa Mwanza, walipata taarifa kutoka vyanzo vyao kwamba, kuna mfanyakazi anatuhumiwa kuomba rushwa kwa mwajiri.

"Baada ya kupata taarifa hiyo, tuliwasilisha kwenye vyombo vya dola na tunawashukuru sana TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) walifanya kazi nzuri na kufanikiwa kumkakata mfanyakazi huyo ambaye alikuwa ameenda kuchukua rushwa kwa mwajiri," alisema Lulu.

Vilevile, aliwataka waajiri wasijishirikishe na baadhi ya wafanyakazi ambao siyo waadilifu kwa kuwa watachukuliwa sheria kali ikiwamo kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

Alisema kulipa mafao kwa mwanachama aliyetimiza vigezo ni matakwa ya kisheria kwenye shirika hilo na kwamba hahitaji kutoa rushwa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Maendeleo ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Shariff Ali Shariff, akitoa maelezo ya eneo la uwekezaji Micheweni Pemba alipofanya ziara ya kutembelea eneo hilo jana. **PICHA: IKULU**

## Mbowe ataja iliko hatima kina Mdee

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema hatima ya wabunge waliokata rufani baada ya kuvuliwa uanachama wa chama hicho, itajulikana baada ya kuketi kwa vikao stahiki vya chama hicho.

Amesema kuwa baada ya wabunge hao kukata rufani, wanaamini kwamba uongozi wa juu wa chama hicho utakapoketi kwa ajili ya kuamua hatima yao, utatenda haki kwa kila mtu.

Mbowe alitoa kauli hiyo katika hotuba yake ya juzi kuhusu masuala mbalimbali, ikiwamo yanayohusu Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28 mwaka jana.

"Chama chetu bila kuwahusisha viongozi wa chama na bila uamuzi wa chama, mama na dada zetu waliapishwa katika mazingira ya kutatanisha na bila kuidhinishwa na chama. Walikata rufani.

"Vikao stahiki vya chama vitakaa wakati mwafaka na kusikiliza rufani zao na nina hakika, haki itatendeka," alisema Mbowe.

Kuhusu Mbunge wa NKasi Kaskazini, Aida Kenani, na baadhi ya madiwani Mkoa wa Rukwa walioapa baada ya uchaguzi huo licha ya chama hicho kuweka katazo, Mbowe alisema nao watajadiliwa kwa wakati mwafaka na uamuzi utatolewa.

"Nguzo kuu ya chama chochote cha siasa ni nidhamu ambayo hujengwa kwa kuheshimu misingi ya chama na inayosimikwa na katiba, chama kitawasikiliza na kuchukua uamuzi stahiki kwa wakati mwafaka zaidi," alisema Mbowe.

Akizungumzia ushirika kati ya chama hicho na ACT-Wazalendo, Mbowe alisema walikubaliana kwa pamoja kuupinga uchaguzi huo, lakini hawakushirikishwa katika uamuzi mwingine ulioendelea ikiwamo kuunda serikali ya umoja wa kitaifa visiwani Zanzibar.

# Majaliwa azindua meli mpya Ziwa Nyasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua rasmi safari ya meli mpya ya MV Mbeya II itakayotoa huduma katika Ziwa Nyasa nchini na nchi jirani za Msumbuji na Malawi.

Meli hiyo yenye thamani ya Sh. bilioni 9.1, ni mwendelezo wa mikakati ya serikali kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria kwa lengo la kuboresha uchumi.

Akizindua safari za meli hiyo jana katika Bandari ya Mbamba Bay wilayani Nyasa, Majaliwa, aliwataka wananchi waitunze meli hiyo ambayo imejengwa na Kampuni ya Kitanzania ya Songoro Mrine.

Waziri Mkuu alisema Tanzania imezungukwa na nchi nane ambazo zinategemea kupata bidhaa mbalimbali kutoka nchini, hivyo wananchi wamie fursa ya uwapo wa meli hiyo kufanya biashara.

Alisema wananchi hawawezi kupata maendeleo bila serikali kujenga miundombinu kama ya meli, barabara, bandari, hivyo akawataka waitumie vizuri kwa ajili ya kukuza uchumi wao.

"Serikali inajenga vitu kwa maendeleo ya watu na kwa kuzingatia hilo, serikali imewekeza fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu itakayowanufaisha kiuchumi kama meli," alisema.

Waziri Mkuu aliagiza kuwe na kanzidata ya mafundi chipukizi wa Kitanzania wanaoshiriki katika ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati kama meli na madaraja makubwa.

Alisema kanzidata hiyo itaiwezesha mafundi hao chipukizi kutambuliwa kwa lengo la kuwaendeleza zaidi na kuwa na ujuzi ili baadaye wapewe miradi ya ujenzi.

Waziri Mkuu alikagua hali ya ujenzi wa mradi wa barabara ya Mbinga-Mbambabay yenye urefu wa kilomita 66 ambayo ujenzi wake umekamilika. Alisema ameridhishwa na ujenzi wake.

"Nimekuja na barabara hii ninateleza tu, wakati ule ulikuwa unatembea katika mawe, makorongo, lakini sasa unalala tu. Ninaipongeza Kampuni ya CHICO kwa ujenzi wa mradi huu," alisifu.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema ujenzi wa barabara hiyo ni kutimiza ndoto za Rais John Magufuli za kuboresha miundombinu.

Alisema kukamilika kwa barabara hiyo pamoja na kuanza kwa safari ya meli, ni ukombozi wa kiuchumi kwa wananchi wa Wilaya ya Nyasa na ukanda mzima wa kusini.

Kasekenya alisema Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itahakikisha inasimamia kikamilifu bandari katika kukusanya mapato yake kwa njia ya kielektroniki, ili zijiendeshe na kwamba haitamvumilia mtendaji yeyote atakayekwenda tofauti.

Meneja wa Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Ruvuma, Alinanuswe Lazeck, alisema ujenzi wa barabara ya Mbinga-Mbamba Bay yenye urefu wa kilomita 66 umegharimu Sh. bilioni 129.361.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari, Deusdedit Kakoko, alisema katika Ziwa Nyasa kuna jumla ya bandari 15. Kati yake, sita ziko mkoani Ruvuma, sita ziko mkoani Njombe na tatu ziko mkoani Mbeya.

Alisema katika kuboresha usafiri Ziwa Nyasa, serikali ilitoa Sh. bilioni 20.1 ambazo zimetumika katika kujenga meli tatu ambazo kati yake, mbili ni za mizigo MV Ruvuma na MV Njombe kwa thamani ya Sh. bilioni 11 na meli ya abiria na mizigo ya MV Mbeya II kwa Sh. bilioni 9.1.

## Waziri aagiza uteuzi wajumbe mabaraza ya ardhi ya wilaya

**Na Munir Shemweta,** LINDI

KATIKA kusogeza huduma za mabaraza ya ardhi na nyumba katika wilaya mbalimbali nchini, serikali imewaelekeza makatibu tawala wa mikoa kuhakikisha wajumbe washauri wa mabaraza hayo wanateuliwa ili kuhudumia wilaya zisizokuwa na mabaraza na kuondoa kero kwa wananchi kutembea umbali mrefu kuzifuata huduma hizo.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alitoa agizo hilo jana mkoani Lindi alipozungumza na watendaji wa sekta ya ardhi, uongozi wa Mkoa wa Lindi na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serilali kupitia kodi ya pango la ardhi. Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, alisema mkoa wake una baraza moja la ardhi na nyumba linalohudumia wilaya zote tano za mkoa huo, jambo alilolieleza kuwa limekuwa likileta usumbufu na kero kwa wananchi kutembea umbali mrefu.

"Mkoa wetu una baraza moja tu la ardhi na nyumba la wilaya linalohudumia wilaya za mkoa huu, fikiria mtu anatoka Liwale kuja hapa umbali wa kilometa 250, ni kumuumiza mwananchi," alilalamika Mkuu wa Mkoa huyo.

Kwa sasa kuna jumla ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 57 yanayotoa huduma nchini wakati sheria inataka kuwa na mabaraza 139, jambo linalosababisha baadhi ya wilaya kukosa huduma hiyo na kuwafanya wananchi kuzifuata huduma kwa kutembea umbali mrefu.

Dk. Mabula alisema baada ya serikali kuona wananchi wanapata shida ya kuzipata huduma za mabaraza ya ardhi, sasa imeamua kuwaelekeza makatibu tawala wa mikoa kuteua wajumbe washauri wa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya sambamba na wakurugenzi wa halmashauri kutakiwa kutenga ofisi itakayoendesha mashauri na kuwa na watumishi kama vile makarani, ili kuwawezesha wenyeviti kufanya kazi kulingana na mahitaji ya wilaya husika.

"Pamoja na kuwa na Mabaraza ya Ardhi katika wilaya mbalimbali, tumeona bado kuna 'gape' (pengo) mahali hasa zile wilaya ambazo hazina mabaraza ya wilaya, maana baraza la wilaya moja linahudunia wilaya tatu," alisema.

Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kwa mujibu wa sheria Na. 2 ya mwaka 2002 lina wajumbe wasiozidi saba na watatu kati yao ni wanawake na kuteuliwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutokana na mapendekezo ya mkuu wa mkoa kutoka katika eneo la wilaya husika.

# Wizara yamweka mtegoni Manara

**Na Thobias Mwanakatwe**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imemtega Msemaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Haji Manara, jinsi atakavyosajili ardhi na mali aliyozawadiwa wakati wa harusi yake iliyofanyika mwishoni mwa mwaka jana.

William Lukuvi amemwingiza kwenye mtego huo Manara alipohojiwa juzi wakati wa kipindi cha Dakika 45 cha ITV, aliposema siku ya harusi ya Manara Kampuni ya ASAS inayotengeneza maziwa mkoani Iringa, ilimzawadia ardhi eneo la Kigamboni jijini Dar es Salaam ambayo haina hati.

"Tunamsubiri Haji (Manara) atakuja kwetu kusajili hati, hatumlazimishi lakini tunataka tumuone Haji japo tunajua huko nyuma ana mali zake na familia yake. Tunataka tumuone atasajili namna gani maana bila yule mke, ndoa isingekuwapo na zawadi isingekuwapo," alisema.

Lukuvi alisema Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 Sura ya 29 kifungu cha 58, inatoa haki kwa kila mwanandoa awe mume au mke kumiliki mali binafsi iwe zile alizochuma kabla ya ndoa na hata akiwa kwenye ndoa.

Hata hivyo, Lukuvi alisema siyo lazima mali iliyopatikana isajiliwe kwa majina mawili "maana unaweza kuwa na mali yako kabla ya ndoa na ukaimiliki peke yako".

"Umiliki wa hati ya mali wa pamoja hauna hisa, unaweza kuandika majina hata ya wanandoa watatu, wewe muislamu una wake watatu, lakini mmoja akitangulia maana yake hisa zimebaki za wengine," alifafanua.

Lukuvi alisema katika kuzingatia uwapo wa migogoro ya ardhi yenye chimbuko la kifamilia, Sheria ya Ardhi inatoa fursa kwa wanandoa kumiliki ardhi kwa pamoja na hati miliki ya pamoja.

Aliongeza kuwa takwimu zinaonyesha kuwa migogoro mingi ya ardhi baina ya wanafamilia hujitokeza pale ndoa zinapofika ukomo.

"Tunashuhudia watoto na kinamama wanakuja kushtuka, lakini hata bila wosia, ndugu wakikaa kwenye vikao wanagawa mali, wale wasimamizi wa mirathi wakiwa hawatendi haki kwa wale wanaostahili kupata faida kutokana na mali za ndugu zao wanasimamia mirathi miaka 10 hadi 20, hakuna mahesabu, ni tatizo," alisema.




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, Gasper Balyomi (kushoto), akimkabidhi funguo za gari Mkuu wa Shule ya Sekondari Tunduru, Limia Ausi, katika hafla fupi iliyofanyika shuleni hapo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. **PICHA: STEVIE CHINDIYE**

# Mtoto adaiwa kujinyonga akitumia sweta

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MWANAFUNZI wa Shule ya Mchepuo wa Kingereza ya Royal Vision ya Jijini Arusha, Junior Calvin (11), anadaiwa kukatisha uhai wake kwa kujinyonga akitumia kipande cha kamba ya sweta juu ya paa la maliwato.

Hata hicho kifo cha mtoto huyo kinaacha maswali yasiyo na majibu hasa kutokana na hatua alizopitia hadi kuchukua uamuzi huo mgumu.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Kamishna Msaidizi, Salum Hamduni, alithibitisha jana taarifa za kudaiwa kujiua kikatili kwa mtoto huyo.

Kwa mujibu wa Kamanda Hamduni, tukio la mtoto huyo kujinyonga lilifanyika Januari 4, mwaka huu, katika Kata ya Sinoni jijini hapa majira ya saa 10 jioni.

"Bado chanzo cha kujinyonga mtoto huyo hakijafahamika, hivi sasa tunachunguza, lakini inaelezwa kwamba mama mzazi wa Calvin, aitwaye Omega Munuo, majira ya alasiri alimpashia mtoto wake maji ili akaoge na alipomaliza, alimwita na kumwelekeza kwenda bafuni kuoga.

"Baada ya kumwelekeza kwenda kuoga, mama mzazi wa Calvin aliendelea kumwandalia chakula mwanawe ili atakapotoka bafuni, wakae na kula pamoja, lakini alistaajabu ukimya wa muda mrefu wa Calvin na muda aliotumia kukaa bafuni na ndipo alipochungulia bafuni na kukuta mtoto kasimama juu ya ndoo, akiwa na kamba shingoni iliyofungwa juu ya paa la bafu (maliwato)," alisimulia.

Alisema mwili wa mwanafunzi huyo umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Akizungumzia tukio hilo, mama Mzazi wa marehemu, Omega Munuo, alisema hakuwa na ugomvi wowote kati yake na mwanawe na wala hakuwa amegombeza.

"Hata siamini kwa sababu nilikuja Arusha, kwa ajili ya kusherehekea Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya na nimwone mwanangu kabla ya kufunguliwa shule Januari 11 mwaka huu.

"Mwanangu wa pekee, ameniacha katika majonzi, tulikuwa tukicheka tangu asubuhi na alinitandikia na kitanda changu, kumbe ilikuwa ishara ya kuniaga," alisema.

Mtoto huyo alikuwa akiishi na bibi yake ambaye ni mama mzazi wa Omega.

Bibi huyo, Glory Munuo, aliyekuwa akiishi naye, alidai kuwa enzi za uhai wake, hakuwahi kuwa mtukutu, aliishi maisha ya kumpenda pamoja na kujituma bila kupigiwa kelele.

"Mjukuu wangu nimemlea tangu akiwa na miezi tisa hadi kufikia hapa, nimesikitishwa na taarifa za kifo chake, kwa sababu aliniaga akaondoka na mama yake mdogo kuja kwa mama yake, cha ajabu ninapata taarifa mbaya za mjukuu wangu," alisema Glory.

# Mradi wa mabilioni Soko la Kimataifa Songwe wakwama

**Na Thobias Mwanakatwe**

MRADI wa Soko la Kimataifa la Mazao Kakozi uliopo wilayani Momba mkoani Songwe ambao utagharimu Sh. bilioni 8.645, umekwama ukiwa umefikia asilimia 34 ya utekelezaji wake.

Kukwama kwa mradi huo kumebainika baada ya Mbunge wa Momba, Condester Sichalwe, kufanya ziara kujionea maendeleo ya ujenzi wa soko hilo ambalo lipo pembezoni mwa barabara kuu ya Tunduma-Sumbawanga.

Kazi za ujenzi ilipangwa kuanza Januari 2019 na kukamilika Januari mwaka huu, lakini umechelewa kwa takribani miezi 12.

Msimamizi Msaidizi wa mradi huo, Caroly Sakaya, alimweleza mbunge huyo kuwa hatua iliyofikiwa hadi Desemba 30 mwaka jana, ni asilimia 34 tu huku serikali ikiwa imetoa zaidi ya Sh. bilioni tatu kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Adrian Jungu, alisema hawana uhakika na muda wa kukamilika kwa mradi huo kama wataendelea kupata fedha kidogo kutoka serikali kuu.

Jungu alisema mtiririko wa upataji fedha toka serikali kuu ndiyo unachangia kuchelewa kwa kazi za ujenzi.

Mkurugenzi huyo alizitaja sababu mbili kuu zilizokwamisha mradi huo kutokamilika kwa wakati kuwa ni mkandarasi mshauri, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, kutokuwapo eneo la ujenzi kwa muda mrefu, hivyo kusababisha ucheleweshaji wa maandalizi ya mahitaji ya vifaa vya ujenzi na kusababisha kazi kuchelewa kumalizika kwa wakati.

Mkurugenzi huyo aliitaja sababu ya pili kuwa ni udhaifu kwenye idara yake ya ununuzi, wakilazimika kuwaondoa baadhi ya maofisa wake kutokana na kile alichodai uwezo mdogo.

"Mradi huo unatekelezwa kwa utaratibu wa 'Force Account', ambapo mteja ndiye mwenye fedha na ndiye anahusika kufanya kazi zote za manunuzi, akitumia mafundi wanaopatikana maeneo ya jirani na mradi, wakati mhandisi mshauri hutoa ushauri wa kitaalamu tu," alisema.

Msimamizi kutoka mhandisi mshauri wa mradi huo, Lameck Owit, alikanusha wao kuwa kikwazo akisema wanakuwapo eneo la mradi muda wote na kuanzia Juni mwaka jana wamekuwapo eneo hilo wakifanya vikao kuhusu kazi zinazotakiwa kufanyika na kutoa ushauri wao wa nini kifanyike.

"Hakuna mtu mwenye maamuzi ya mradi uende au usiende kama mwenye fedha, sisi tunashauri, alisema Owit katika mahojiano na Nipashe.

Mbunge wa Momba, Sichalwe, alibainisha kuwa kitengo cha ununuzi cha halmashauri hiyo ndiyo chanzo cha kuchelewa kwa mradi huo.

"Tatizo lipo kwa DED na watu wake wa ununuzi kwani kinachokwamisha kazi kuendelea ni vifaa kutokuwapo eneo la kazi wakati fedha zipo," alisema.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Oscar Mwilongo, ambaye mradi huo upo chini ya idara yake, alisema mabadiliko ya mfumo wa utekelezaji mradi huo kutoka kutumia mkandarasi kwenda kwenye 'force account', yamechangia kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huo.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene (kushoto), akimkabidhi cheti cha kutambua ujasiri na utendaji kazi, askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Koplo Denis Minja, aliyeokoa maisha ya mtoto wa miaka miwili aliyetumbukia kwenye shimo la choo Mjini Karagwe. Tukio hilo limefanyika jana, Ofisi za Makao Makuu ya Wizara hiyo Mtumba, jijini Dodoma. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

## Shein aahidi kuipaisha Mzumbe kimataifa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

RAIS mstaafu wa awamu ya saba Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesimikwa rasmi kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe (MU) na kuahidi kukiunganisha na vyuo vikuu vingine vya ndani na nje ya nchi, ili kuimarisha masuala ya utafiti, taaluma inayoenda na wakati na kutoa ushauri wa kitaaluma.

Dk. Shein alitoa ahadi hiyo jana mkoani Morogoro baada ya kusimikwa na kukabidhiwa vitendea kazi na aliyekuwa Mkuu wa chuo hicho, Jaji Mkuu mstaafu Barnabas Samatta.

Alisema ili Mzumbe ipate hadhi ya kitaifa na kimataifa, ni lazima iwe na uwezo mkubwa wa kutekeleza majukumu yake makuu ya msingi; kwanza kutoa taaluma inayokwenda na wakati ambayo itawezesha kuwa chuo kitakachoweza kuchangia soko la ajira.

Dk. Shein aliahidi kuhakikisha anakiunganisha chuo hicho na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), ili kuleta mafanikio katika nyanja ya kukuza taaluma na kubadilishana uzoefu kwa lengo la kuongeza soko la ajira nchini hasa kwa vijana.

Alisema kuwa pamoja na kuwapo kwa vikwazo mbalimbali, aliutaka uongozi kuendelea kuwa karibu na jamii katika kutatua matatizo walionayo, akipongeza namna walivyosaidia kukarabati Shule ya Sekondari Mzumbe.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Lughano Kusiluka, alisema kuwa pamoja na kuwapo kwa vikwazo mbalimbali, pamekuwapo mafanikio mengi ndani ya kipindi cha miaka 12 ya uongozi wa Jaji Samatta, ikiwa ni pamoja na ongezeko la wanafunzi kutoka 5,176 mwaka 2009 hadi 11,967 mwaka 2020 (asilimia 57).

Profesa Kusilika alisema katika kipindi hicho, wanataaluma wa shahada ya uzamivu (PhD) wameongezeka kutoka 45 hadi kufikia 122 (asilimia 85).

Alipongeza serikali kwa kuwekeza katika chuo hicho kupitia miradi mbalimbali uiwamo mradi mkubwa wa ujenzi wa hosteli kwa gharama ya Sh. bilioni 6.5 na tayari umekamilika.

Novemba 24 mwaka jana, Dk. Shein aliteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe na Rais Dk. John Magufuli baada ya Jaji Mkuu mstaafu Samatta kumaliza muda wake baada ya kukitumikia chuo hicho kwa miaka 12.

# Mahakama yamkuta na kesi ya kubaka mtoto

**Na Joctan Ngelly Geita**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita, imebaini mkazi wa Nyankumbu, Ben Maganga (26), ana kesi ya kujibu baada ya Upande wa Mashtaka kufunga ushahidi wake.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashtaka mawili ya kubaka na kumpa mimba msichana mwenye umri wa miaka 15 ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya Nyarugusu.

Mshtakiwa huyo ambaye yuko nje kwa dhamana, alifikishwa mahakamani majira ya saa tatu asubuhi na kupandishwa kizimbani majira ya saa nane mchana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Samweli Maweda, na aliposomewa mashtaka yake mawili, alikana kuhusika na makosa hayo.

Uamuzi huo wa kumkuta na hatia ulitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, baada ya Upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wake.

Maweda alisema Upande wa Jamhuri, ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Daniel Masambu, ulipeleka mahakamani huko mashahidi wanne na vielelezo vitatu.

Alisema mahakama yake imemwona mshtakiwa kuwa ana kesi ya kujibu na kumtaka ajitetee.

Hakimu Maweda alimuuliza mshtakiwa kama atakuwa na shahidi au kielelezo na mshtakiwa huyo alijibu kuwa atajitetea peke yake na pia hatakuwa na kielelezo chochote.

Upande wa Jamhuri uliomba tarehe nyingine kwa ajili ya mshtakiwa huyo kutoa utetezi wake mahakamani huko.

Hakimu Maweda aliahirisha kesi hiyo hadi Febuari 4 mwaka huu kwa ajili ya mshtakiwa huyo kutoa utetezi wake mahakamani huko.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Masambu, alidai mahakamani huko kuwa tarehe na muda usiyojulikana kati ya Desemba mwaka 2019 na Januari 27, 2020 huko Nyankumbu, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimbaka na kumpa ujauzito msichana mwenye umri wa miaka 15 ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Nyarugusu kinyume cha sheria.

HABARI KITAIFA

## TCRA yaifungia wasafi Tv

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), imekifungia kwa muda wa miezi sita kituo cha televisheni cha Wasafi kwa madai ya kukiuka kanuni za urushaji matangazo ya moja kwa moja.

Kaimu Mkurugenzi wa TCRA, Johanes Kalungule, alisema jana kuwa ukiukwaji huo ulifanyika Januari Mosi mwaka huu, kituo hicho cha televisheni kiliporusha maudhui yaliyomwonyesha msanii Gift Joshua, maarufu Gigy Money, akicheza katika mitindo iliyoonyesha utupu wake.

Kalungule alisema kosa hilo ni kinyume cha kanuni za utangazaji, hivyo kuanzia muda uliotolewa uamuzi huo, Wasafi TV imetakiwa kusitisha matangazo yake na kuomba radhi.

"Pia, TCRA imesitisha utoaji wa huduma za utangazaji za Wasafi Tv kwa muda wa miezi sita kuanzia Januari 6, 2021 hadi Julai 6," alisema.

Aliongeza kuwa iwapo Wasafi Tv itashindwa, itakataa au kukaidi uamuzi huo, hatua zaidi za kisheria na za kiudhibiti zitachukuliwa dhidi yao.

Kutokana na tukio hilo, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), nalo limemfungia kwa muda wa miezi sita msanii Gigy Money. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Katibu Mtendaji wa BASATA, Matiko Mniko, msanii huyo alifanya kitendo hicho huku akifahamu kuwa tukio linarushwa mubashara na televisheni ya Wasafi na kuonwa na watu wa rika mbalimbali, hivyo kwenda kinyume na kanuni za baraza za mwaka 2018.

Aliongeza kuwa adhabu hiyo itadumu kwa miezi sita na amefungiwa kujihusisha na shughuli za sanaa ndani na nje ya nchi na anatakiwa kulipa faini Sh. milioni moja na adhabu hiyo imetolewa kwa mujibu wa kanuni ya 64(1)(a)-(1) ya Kanuni za Baraza za Mwaka 2018.

Baraza hilo pia limewakumbusha wasanii wote nchini kufanya shughuli za sanaa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

# Tito, wenzake wahukumiwa kulipa fidia milioni 17/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewahukumu Ofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti na mwenzake, Theodory Giyani (36), mtaalamu wa mfumo wa kompyuta, kulipa fidia ya Sh. milioni 17.3 baada ya kupatikana na hatia ya kosa la kuongoza genge la uhalifu.

Kadhalika, mahakama hiyo imewaamuru washtakiwa kutokutenda kosa la jinai kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia jana iliposomwa hukumu hiyo.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega, baada ya washtakiwa kuingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) ya kukiri makosa yao.

Hakimu Mtega alisema, mahakama yake bila kuacha shaka imewaona washtakiwa wana hatia ya kosa la kuongoza genge la uhalifu.

"Mahakama hii imewaona washtakiwa mna hatia ya kosa la kuongoza genge la uhalifu wa kupangwa, inawahukumu kulipa fidia ya Sh. 17,354,535 kwa serikali, pia inawaamuru kuanzia leo (jana), msitende kosa la jinai ndani ya mwaka mmoja," alisema Hakimu Mtega.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon.

Kadushi alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya uamuzi kutokana na washtakiwa kukiri mashtaka yao.

Kadushi aliendelea kudai kuwa awali washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na mashtaka matatu, lakini baada ya kufanya makubaliano na DPP wamefutiwa mawili na kubakisha moja ambalo ni kuongoza genge la uhalifu.

Wankyo alidai kuwa kati ya Februari mosi na Desemba 17, 2019 jijini Dar es Salaam na mahali tofauti nchini Tanzania, mshtakiwa Magoti, Giyani na wenzao ambao hawajafikishwa mahakamani, walishiriki makosa ya uhalifu wa kupanga kwa kumiliki programu za kompyuta iliyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kufanya uhalifu na kusababisha kujipatia Sh. 17,354,535.

Washtakiwa kwa nyakati tofauti waliomba mahakama hiyo kuwapunguzia adhabu kwa sababu ni vijana wadogo na wanategemewa na familia zao na walionyesha ushirikiano tangu siku ya kwanza walipofikishwa mahakamani hapo.



Baadhi ya wanachama wa kikundi cha Moro Family cha mjini Morogoro, wakiwa na watoto yatima wa Kituo cha Rayah Islamic Centre kilichopo Bigwa mjini humo, walipokwenda kutoa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo unga wa mahindi na sabuni, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamwomba mbunge wao kumalizia ujenzi zahanati

**Na Gurian Adolf,** NKASI

BAADHI ya wanaume Kijiji cha Matala, wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wamemwomba Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, Aida Khenan (CHADEMA), awasaidie kumalizia ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho kuwasaidia wake zao kuondokana na usumbufu wa kutafuta huduma za uzazi salama wanapotaka kujifungua.

Ombi hilo walilitoa jana kwenye mkutano wa hadhara wakati mbunge huyo alipofika katika kijiji hicho kufanya mkutano wa hadhara wa kuwashukuru wapigakura wake na kusikiliza kero zinazowakabili.

Mmoja wa wakazi, Paul Kiozya, alimwambia mbunge huyo kuwa moja ya kero inayokikabili kijiji hicho ni ukosefu wa zahanati hali inayowalazimu kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katika vijiji jirani.

Alisema kero zaidi ni wanawake wanapo lazimika kutembea umbali mrefu wakiwa katika hali ya uchungu wa kujifungua na wakati mwingine wakilazimika kutembea kwa miguu usiku huku mvua ikinyesha.

Kiozya alisema wanakijiji wamechangishana fedha pamoja na nguvu kazi na kujenga jengo la zahanati ya kijiji kufikia usawa wa lenta, lakini wameshindwa kumalizia kuezeka kwa zaidi ya miaka miwili sasa.

Walimwomba mbunge huyo awasaidie ili wapate zahanati.

Mkazi mwingine, Lenatus Kasamya, alisema changamoto nyingine inayowakabili ni ukosefu wa majisafi kwa kuwa miradi ya maji iliyotekelezwa miaka ya nyuma haitoi huduma hiyo kwa muda mrefu na hulazimika kutumia ya visima vifupi wanavyojichimbia wenyewe ambavyo si salama.

Kwa upande wake Mbunge Khenan aliwashukuru wakazi hao kwa kura na kuibuka mshindi katika uchaguzi mkuu uliopita, pia aliwataka kujituma kufanya kazi kwa bidii, ili kupata maendeleo na kuwaahidi kero zote walizozitoa amezichukua na anazitafutia majibu pamoja na ufumbuzi.

DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

**SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATAFUTA MTOA HUDUMA WA BIMA YA AFYA KWA WAFANYAKAZI WA SHIRIKA LA DANISHI.**

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI/WATOA HUDUMA WENYE NIA KULETA ZABUNI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 05.01.2021 HADI TAREHE 11.01.2021 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255625482649 au barua pepe jackson.maseke@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA TAREHE 12.01.2021 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI YA DANISHI.**

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI KIBONDO VINGINEVYO NI BATILI.**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tiketi kielektroniki zianze kimaridhiano

**MAMLAKA** ya Udhibiti wa Usafirishaji Nchi Kavu (LATRA) imeagiza mabasi ya wasafirishaji abiria kuanza kutoa huduma ya kuuza tiketi kwa mfumo wa kielektroniki, kuanzia leo.

Hilo ni jambo jema linalorahisisha na kuwawezesha wananchi kununua tiketi kwa urahisi na kupunguza usumbufu, gharama za kuzifuatilia pamoja na kuepusha kuibiwa hasa kwa wageni wanaozifuatilia tiketi hizo vituoni.

Lakini ni jambo jema pia kudhibiti uhalifu hasa unaotokana na ulanguzi wa tiketi hizo unaotokea msimu wa sikukuu hasa za mwisho wa mwaka ikiwamo na Noeli pia na hata kipindi cha Pasaka ambacho baadhi ya watu hupenda kurudi nyumbani kusherehekea na familia zao.

Kusisitiza uwepo wa tiketi za kielektroniki ni mwendelezo wa mipango ya serikali ya kuboresha sekta ya usafirishaji na kuifanya pia ichangie kwenye uchumi wa nchi kwa kupanua wigo wa vyanzo vya mapato, ikikumbukwa kuwa serikali imeanza na kukatisha tiketi kielektroniki kwenye usafiri wa treni.

Tunaipongeza serikali kwa mipango ya kupunguza adha wanayoipata wakazi wa maeneo mbalimbali hasa wa mbali na stesheni au mawakala wa tiketi ambao wanahitaji kupata huduma hiyo hivyo kuufanya uuzaji wa tiketi kuwa rahisi na unaopatikana kwa wakati, lakini ni jambo ambalo linahitaji maandalizi zaidi na ushiriki wa pande zote wadau wa usafirishaji, LATRA, Mamlaka ya Mapato (TRA), mawakala, abiria na wenye kutoa huduma za mtandao.

Anawezekana utaratibu huo unakuwa na changamoto zake kwa kusababisha wasafirishaji hawajaridhika na pia hakujawa na maelekezo ya kutosha kutoka pande zinazosimamia mapato hasa TRA na LATRA, hivyo ni vyema kuangalia upya utaratibu huo na kuufanyia kazi kikamilifu ili kuziridhisha pande zinazohusika ili kuepusha wenye mabasi kugoma na kuhatarisha abiria kukwama au kulala vituoni kutokana na kukosa magari.

Tunaona kuwa ni vyema kutoa huduma hizo kwa hatua na uanzishaji wa mfumo wa mabasi kwa njia ya tiketi za mtandao utengenezwe kwa namna ambayo pande zote zitanufaika kwa sababu kuendesha huduma ya usafiri nako kuna gharama kubwa na wakati mwingine wahusika wanaweza kupata changamoto ya idadi ndogo ya wasafiri kwa vile si wakati wote watu hutumia vyombo hivyo.

Licha ya LATRA kuwa na nia njema ya kuanza kutekeleza agizo hilo kwa mabasi yakiwamo yanayosafiri kati ya Dar, Tanga, Lindi na Tanga hadi Arusha, msimu huu unaweza kuwatatiza wanafunzi wanaorudi shuleni.

Lakini, pia bila kuwa na utaratibu unaoeleweka na kukubalika kuna uwezekano wa mamia ya abiria walioko mikoani kukwama kurejea kazini hasa wanaosafiri kati ya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Tanga na Dar es Salaam.


Kabla ya kuingia kwenye mkwamo ni wakati wa wadau wakiwamo wamiliki, watoa huduma za mitandao, TRA, LATRA na wengine kusikilizana, kutoa na kusikiliza maoni ya pande zote na kuanza utaratibu mpya baada ya makubaliano.

Tunawakumbusha wasafirishaji kuwa hawana sababu ya kuhofia usafirishaji unaotumia njia za kielektroniki kwa vile zama hizi kila jambo linafanywa kwa njia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Tunawakumbusha watoa huduma kuwa ni wakati muafaka wa kujipanga na kuanza kazi, ikizingatiwa kuwa kama LATRA, ilivyoeleza, stendi mpya ya Mbezi jijini Dar es Salaam ni ya kimataifa, hivyo tiketi za mtandaoni itakuwa utaratibu endelevu unaohusisha wasafiri wa nje ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi, walezi walinde vipaji vya watoto

**KIPAJI** ni uwezo wa kipekee mtu anachozaliwa nacho yakiwa ni maarifa ya kufanya jambo fulani kwa maarifa na ubunifu wa hali ya juu bila kufundishwa au baada ya kufundishwa kidogo na kinaweza kuwa cha kimwili au cha kiakili.

Lakini pia, kipaji kinaweza kuendelezwa au kudumazwa iwapo mzazi ama mlezi hawataweza kutambua uwezo ama kipaji cha mtoto wao na kutumia fursa zilizopo kukiendeleza.

Kwa kawaida, wazazi au walezi wako makini, hutambua vipaji vya watoto wao mapema na kuanza kuviendeleza, kwa kuwapa nyenzo mbalimbali ambazo huwasaidia katika kuboresha uwezo walio nao.

Katika kundi hilo, wapo wazazi na walezi ambao wana malengo juu ya kitu gani wanapenda watoto wao wafanye wawapo wakubwa bila kujali kwamba wanaweza kuua vipaji vya watoto wao.

Vipo baadhi ya vipaji kama kuimba na kucheza muziki, ambavyo, wazazi na walezi huviona upotoshaji wa maadili, hivyo hawako tayari kuviendeleza na wanataka wafuate kile ambacho wao wanafanya.

Hata hivyo katika dunia ya leo, wazazi na walezi wa aina hiyo wanatakiwa kubadilika na kwenda na wakati kwa kuruhusu na kuendekeza vipaji vya watoto wao ili viweze kuwanufaisha katika maisha yao ya baadaye.

Kimsingi, mtoto anatakiwa kuandaliwa maisha yake ya sasa na ya baadaye hasa kwa kutambua na kuendeleza kipaji chake, kwa kuwa anapofikia umri wa kujielewa ana haki ya kufanya maamuzi kuwa anapenda nini ilimradi ni jambo jema kisheria, kidini, kiafya na kijamii.

Hivyo, kutambua kipaji cha mtoto na kukiendeleza ni jambo la msingi, kuliko kumlazimisha asomee taaluma ambayo haipendi, ingawa baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia hiyo ya kutaka watoto wasomee kile ambacho wanataka.

Kumuacha mtoto aamue anachotaka kukisomea au kuendeleza kipaji chake, ni jambo la msingi kwa kuwa pia ana malengo ya baadaye, hivyo aendelezwe kipaji chake au aachwe asomee kile anachokitaka.

Hapa kuna mambo mawili ya kuzingatia, kufuatilia maendeleo ya mtoto na kubaini uelekeo wake ili kubaini na kumhimiza aongeze kasi ili afikie kile anachokitafuta kwa baadaye.

Wakati mwingine vipaji vya watoto haviendelezwi, kwa sababu mzazi au mlezi anataka watoto wake wawe katika nafasi au kufanya ambayo yawezekana hawayataki.

Kwa kawaida, mzazi au mlezi ni mwalimu wa kwanza, na kwa kiasi kikubwa wanae hujifunza na kuiga mambo mbalimbali kutoka kwake, hivyo anatakiwa pia kuhakikisha anamfundisha masuala muhimu anayopaswa kujifunza.

Hivyo kwa umuhimu huo anatakiwa kumfundisha mtoto wake mambo kadhaa kama matumizi mazuri ya muda, lakini pia kuendeleza kipaji chochote ambacho atakuwa nacho.

Kwenye masuala ya matumizi ya muda, anatakiwa amfundishe kulala na kuamka mapema, kula kwa wakati, kuwahi eneo anakokwenda, kujiwekea ratiba na kuifuata.

Pamoja na hayo, si sahihi sana mzazi au mlezi kumchagulia mtoto mambo ya kusomea, kama mzazi daktari, asilazimishe mtoto naye awe daktari. Unaweza wakati mwingine ana ndoto zake nyingine.

Hivyo watoto waachwe huru kuchagua kile wanachokitaka kusomea kulingana na uwezo wao darasani na jinsi ambavyo wamepanga kutimiza ndoto zao.

Ni vyema wazazi waepuke kuwa chanzo cha kukwamisha watoto, kwa sababu ya kutotambua vipaji vyao, badala yake wawe mstari wa mbele kuvibaini na kuviendeleza kwa kuwa ni njia nzuri ya kuwawezesha kimaisha.

Suala la mtoto kusoma ni la muhimu, lakini inawezekana kuwa na muda wa ziada, hasa maisha nje ya darasa, ambako anaonyesha kipaji chake hasa kwenye michezo.

Lakini baadhi ya wazazi wanaweza kusema kuwa si sahihi mtoto kujihusisha na michezo, kwa madai kwamba, ataacha masomo na kuelekeza nguvu zaidi kwenye michezo.

Ni vyema kuwasaidia ili wafikie azma yao badala ya kuwakataza kwa hofu ambazo wakati mwingine haziwezi kuthibitishwa.

## HABARI KITAIFA

# Tiketi kielektroniki zaleta mkanganyiko

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Joseph Priskus, amesema suala la tiketi za kielektroniki kwa upande wao limekuwa na mkanganyiko kwa kuwa halijatolewa elimu ya kutosha.

Mkanganyiko huo unatokana na taarifa iliyotolewa mwanzoni mwa wiki na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) iliyowataka wamiliki wote wa mabasi ya abiria kutumia tiketi za kielektroniki kuanzia Januari 6 na asiyetekeleza agizo hilo hataruhusiwa kutoa huduma hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Priskus alisema kulitakiwa kutolewe elimu ambayo anadai bado haijatolewa vya kutosha. Alisema LATRA wamekuwa wakitoa elimu hiyo kwa wamiliki wa magari wakati walipaswa kuitoa kwa wafanyakazi wanaohusika na ukataji wa tiketi hizo ambao ni makondakta wa magari.

"Makondakta wa magari ndiyo wanaotakiwa kupewa elimu hiyo kwani asipotoa tiketi TRA watamkamata na kumpiga faini ya hadi Sh. 4,500,000 na LATRA nao watamkamata na kumpiga faini ya Sh. 250,000, hivyo utaona kosa moja mtu anaadhibiwa mara mbili," alisema.

Aliongeza kuwa suala la risiti wameshaongea na Kamishna wa TRA, lakini bado hawajafikia mwafaka wa namna ya kulipa kodi na kwamba kuna ulazima wa kutolewa elimu ya tiketi na risiti ili kuondoa mkanganyiko.

Alisema suala hilo linawachanganya kutokana na LATRA kuita tiketi na TRA kuita risiti.

"Kuna huduma ndogondogo zinazofanywa kwenye gari ambazo zinatucost hela nyingi na hazitolewi risiti kwa kuwa wanaotuhudumia ni watu wasio rasmi wenye vitambulisho vya ujasiriamali na ukiwapelekea TRA hesabu hizo hawawezi kukuelewa, hivyo elimu ya mlipakodi inatakiwa kutolewa kikamilifu," alisema.

Aidha, alisema suala la tiketi za kielektroniki litakuwa na faida kwa serikali, lakini sio kwa upande wao na wameiomba serikali kuwakata asilimia moja kwa kila tiketi kutoka mbili ambazo zimekuwa zikikatwa na LATRA vinginevyo wakubaliane na mahesabu watakayoletewa na wamiliki wa magari.

Alitoa wito kwa mamlaka husika kuweka utaratibu unaoeleweka katika suala la tiketi za kielektroniki kwa kuwa linazua sintofahamu kwa wamiliki wa mabasi kutokana na kuzua mkanganyiko kwa kitu kimoja kutumiwa na mamlaka mbili tofauti.

Mkurugenzi wa Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA) Kanda ya Kaskazini, Solomoni Nkiggi, alisema wamelipokea suala la tiketi mtandao na wanaendelea kutoa elimu kwa abiria ili kuwajengea uelewa jinsi ya kuzitumia. Alisema mpaka sasa kuna baadhi ya wamiliki wa mabasi wameshaanza kutekeleza agizo la kutoa tiketi za kielektroniki ingawa baadhi bado wanasuasua.

"Wengine wanaona bado hakujatolewa elimu ya kutosha kuhusu tiketi hizo, lakini sisi kama CHAKUA tunafurahi kwani kilikuwa ni kilio chetu cha muda mrefu toka mwaka 2012," alisema.

Alisema kuna tatizo linalowakuta abiria kutokana na suala hilo kwa kuwa sio wasafiri wote wenye simu janja, lakini wameiomba serikali kutilia mkazo jambo la kutoa elimu na wao kama CHAKUA watalifikisha kwa abiria.

# Meneja aonja joto ya N/Waziri Maji

**Na Thobias Mwanakatwe**

KASI ya utendaji kazi ya mawaziri na manaibu mawaziri imegeuka kuwa shubiri kwa baadhi ya watendaji kwenye usimamizi wa miradi katika wilaya zao.

Meneja wa Mamlaka ya Maji Mji Mdogo wa Rujewa wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, Victor Mtata, ni miongoni mwa watendaji walioonja jana moto wa Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, baada ya kutoa maelezo ambayo hayakumridhisha kuhusu mradi wa maji Uhamila.

Naibu Waziri alifika katika mradi huo akiwa na viongozi wengine akiwamo diwani, lakini meneja huyo hakuwapo eneo la mradi na kupigiwa simu na waziri kuulizwa na hali ilikuwa hivi:

**Waziri:** Kwenye huu mradi kwa mara ya mwisho umesambaza maji lini.

**Meneja:** Huu mradi wa Uhamila unafanya kazi siku zote ila kuna low voltage ya umeme.

**Waziri:** Mara ya mwisho umetoa lini maji kwa wananchi.

**Meneja:** Ni kila siku wanapata maji mkuu

**Waziri:** Niko na anayeishi hapa, kwa hiyo umeamua kunidanganya si ndio maana yake.

**Meneja:** Hapana huwa tunapeleka maji ila changamoto ni umeme.

**Waziri:** Kwa hiyo low voltage leo imekwisha umegawa maji si ndio.

**Meneja:** Kwanza jana kulikuwa na low voltage mkuu, lakini kutokana na hali ya umeme unakuwa na mawimbi mawimbi ukitulia wana pampu maji.

**Waziri:** Tanesco mnadaiwa shilingi ngapi.

**Meneja:** Tanesco hatudaiwi mkuu

**Waziri:** Ongea na anayeishi hapa ambaye ni mhe. diwani ukiendelea kuongea uongo mimi nitakuadhibu kwa nidhamu za watumishi wa umma kwa sababu unaongea masuala ambayo hayapo. Hebu nikukute pale kituo cha polisi unanisubiria kwanza, nenda sasa hivi namwambia OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya) utawakuta pale watakaokupokea vizuri nikukute hapo.

**Meneja:** Mkuu mimi nipo Musoma mama anaumwa ugonjwa wa kichaa, niko huku mkuu.

**Waziri:** Na wewe ndio umechanganikiwa, maana na wewe unaongea kama kichaa, hayo unayoongea yote ya uongo.


**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
**Company No. 22797**

the bank for your development

## NOTICE FOR CONVENING THE ANNUAL GENERAL MEETING AND EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING

**A: ANNUAL GENERAL MEETING**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT THE ANNUAL GENERAL MEETING OF AKIBA COMMERCIAL BANK PLC SHALL BE HELD ON SATURDAY, 30TH JANUARY 2021 AT DAR ES SALAAM SERENA HOTEL FROM 10:00 A.M. (EAT)**

**AGENDA:**

1.0 NOTICE, CONFIRMATION OF QUORUM AND ADOPTION OF THE AGENDA
2.0 TO CONFIRM THE MINUTES OF THE PREVIOUS MEETING
3.0 TO DISCUSS MATTERS ARISING FROM THE PREVIOUS MINUTES
4.0 TO RECEIVE THE CHAIRMAN'S STATEMENT
5.0 TO RECEIVE AND APPROVE THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER, 2019 TOGETHER WITH THE DIRECTORS' AND AUDITORS' REPORTS THEREON
6.0 TO RECEIVE REPORT ON THE BANK'S PERFORMANCE
7.0 TO RECEIVE UPDATE ON PROJECT OX
8.0 TO RATIFY THE RE-APPOINTMENT/APPOINTMENT OF NEW DIRECTORS AND ACCEPT RESIGNATION OF DIRECTORS
9.0 TO RATIFY THE APPOINTMENT OF EXTERNAL AUDITORS FOR THE YEAR ENDING 31ST DECEMBER, 2020 AND APPROVE THEIR REMUNERATION
10.0 TO SET DATE FOR THE NEXT ANNUAL GENERAL MEETING
11.0 CLOSING REMARKS

**B: EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING OF AKIBA COMMERCIAL BANK PLC SHALL BE HELD ON SATURDAY, 30TH JANUARY 2021 AT DAR ES SALAAM SERENA HOTEL IMEDIATELY AFTER THE ANNUAL GENERAL MEETING**

**AGENDA:**

1.0 NOTICE, CONFIRMATION OF QUORUM AND ADOPTION OF THE AGENDA
2.0 TO RECEIVE AND APPROVE THE PROPOSAL FOR CONVERSION OF SHARES
3.0 TO RECEIVE AND APPROVE THE REVISED MEMORANDUM AND ARTICLES OF ASSOCIATION
4.0 CLOSING REMARKS

**NOTE:**

A. **PAPERS FOR THE MEETING**
Papers for the meetings will be available for collection at the Bank's Registered Offices from Monday, 25th January 2021 and at the venue on the date of the meeting.

B. **OPTION TO JOIN VIRTUALLY**
Shareholders may join the meetings virtually if unable to attend physically, by sending an email to the Company Secretary to register their attendance and obtain meeting access by Thursday, 28th January 2021. The meetings can be accessed virtually only by Shareholders who have registered their attendance in accordance with this notice.

C. **ATTENDANCE BY PROXY**
A Shareholder entitled to attend and vote at these meetings may, if unable to attend in person, appoint a proxy to attend and vote on his/her behalf in accordance with the provisions of the Articles of the Company.

The instrument appointing a proxy must be signed by the respective Shareholder.

The instrument appointing a proxy must be submitted to the Company Secretary at the Banks registered office or via email by 10.00 a.m. Thursday, 28th January 2021.

D. **TRAVEL AND ACCOMMODATION**
Each Shareholder shall be responsible for the cost of their own travel and accommodation.

E. **OTHER INFORMATION**
Shareholders are reminded to confirm/update their personal information with the Company Secretary in order to update the Company Register.

F. **CONTACT DETAILS FOR COMMUNICATION**

Company Secretary
Akiba Commercial Bank Plc
3rd Floor, Amani Place, Ohio Street
P.O. Box 669
**Dar es Salaam**

Tel: 0742 972 072 or 0677 152 000
Email: **cs@acbtz.com or niwaeli.mziray@acbtz.com**

**By Order of the Board**

**Company Secretary**
**6th January 2021**

**Distribution:** Shareholders - Akiba Commercial Bank Plc

**Invitees:** Board of Directors - Akiba Commercial Bank Plc
Senior Management - Akiba Commercial Bank Plc
External Auditors - PricewaterhouseCoopers
Director, Banks Supervision Department - Bank of Tanzania

HABARI KITAIFA

# RC aagiza DED, Ofisa Ardhi wawekwe selo

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

MKURUGENZI Mtendaji na Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, wameagizwa kumlipa mwananchi fidia ya Sh. milioni 3.1 baada ya halmashauri hiyo kutwaa eneo lake na kupima viwanja vya makazi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, baada ya mwananchi huyo, Derefa Christopher, kuangua kilio mbele yake akilalamika kudhulumiwa malipo ya fidia ya shamba lake.

Alisema kuwa kati ya Sh. milioni 4.6 za fidia ya ardhi yake iliyotwaliwa na halmashauri kwa ajili ya kupima viwanja vya makazi, anadai Sh. milioni 3.1 badala ya kulipwa kiwango kinachobaki.

"Mheshimiwa Waziri, nimedhulumiwa shamba langu na mkurugenzi, alinilipa Sh. milioni moja na kila nikidai, ananifukuza kama mbwa na kunikejeli kama si shamba ningefanyaje. Ninaomba unisaidie," alisema.

Kutokana na malalamiko hayo, Jafo alimhoji Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Boniface Magesa, kuhusu madai ya mwananchi huyo na alidai walimrejeshea eneo lake lakini akagoma na kutaka alipwe fedha.

Hata hivyo, Magesa na ofisa ardhi wa halmashauri hiyo aliyefahamika kwa jina moja Mkalipa, walionekana kutupiana mpira kuhusu sakata hilo ndipo Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole, alipoingilia kati na kukiri kudanganywa na vigogo hao kuhusu suala hilo.

"Mheshimiwa Waziri, nilinipotoshwa katika suala hili, walinipa taarifa kuwa walimlipa fidia ya fedha na wakampa eneo jingine kubwa zaidi ya eneo lake," alisema Kipole.


Jafo alionyesha kukerwa na majibu ya vigogo hao, akaagiza wamlipe mwananchi huyo fedha zake Sh. milioni 3.1 kabla ya saa 9:00 alasiri jana akiwa ziarani Buchosa.

"Mzee mtu mzima anatoa machozi, ninaagiza hadi kesho awe amelipwa fedha zake zote na nipate taarifa kabla ya saa 9 leo (jana), mmefanya dhuluma kubwa, mmewadanganya wawakilishi wa Rais mkiwa watumishi wa umma na mmekiuka maadili, lazima niseme ukweli halmashauri hii haipo vizuri kabisa," alisema.

Waziri huyo alisema angekuwa na mamlaka ya kuwasweka ndani, angeagiza wawekwe korokoroni kwa saa tatu ili waone athari ya kuogopa wakati mhasibu akifanya taratibu za kuomba fedha na malipo.

"Mmemdanganya DC na RC aliagiza kwa barua suala hilo lishughulikiwe, mkajibu mmeshamalizana naye, kumbe mzee hajalipwa, ningekuwa na kofia hiyo ningeagiza OCD kamata weka ndani lakini mamlaka hiyo sina," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, aligongomelea msumari akasema sheria ipo na kumwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Sengerema, Mark Marwa, kuwakamata Mkurugenzi na Ofisa Ardhi na kuwasweka mahabusu kwa kuwa sheria inamruhusu.




Meneja Huduma za kadi wa Benki ya NMB, Ednamamu Shobi, akichezesha droo ya tano ya promosheni ya NMB MASTABATA jijini Dar es Salaam. Katikati ni Meneja Mwandamizi Biashara za Kadi wa Benki ya NMB, Lupia Matta na kushoto ni Msimamizi wa Michezo ya kubahatisha kutoka Bodi ya Taifa ya Michezo ya kubahatisha, Joram Matafya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatangaza washindi 40

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetumia jumla ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya washindi 200 wa droo za wiki tano tangu kuanza kwa promosheni ya MastaBATA mwishoni mwa mwezi Novemba, mwaka jana.

Benki hiyo jana ilitangaza washindi 40 wa droo ya 5 ya Kampeni ya NMB MastaBATA, idadi inayofanya jumla ya washindi 200 hadi sasa kujishindia Sh. 100,000 kila mmoja kati ya 400 wanaotarajiwa kuzawadiwa katika kipindi cha kampeni hiyo.

NMB MastaBATA ni kampeni ya miezi mitatu iliyozinduliwa Novemba 24, 2020 na itadumu hadi Februari 2021 kwa kutolewa zawadi mbalimbali zikiwamo pesa, simu janja, jokofu, runinga na safari ya kwenda kupumzika Zanzibar, Serengeti na Ngorongoro.

Akizungumza wakati wa droo ya wiki ya tano iliyofanyika jijini Dares Salaam jana, Meneja Mwandamizi Biashara ya kadi wa NMB, Lupia Matta, alisema kampeni hiyo imeongeza idadi ya watumiaji wapya wa kadi za NMB Mastercard na Masterpass QR kwa asilimia 50.

Matta alibainisha kuwa, NMB MastaBATA na NMB Friday, kampeni mbili zinazochagiza matumizi ya NMB Mastercard na Masterpass QR, zimeonyesha mafanikio makubwa kwa kuongeza idadi ya watumiaji kwa asilimia 50.

"Kumekuwa na zaidi ya asilimia 50 ya watumiaji wapya wanaoingia katika utamaduni wa ununuzi kwa kutumia kadi, idadi ambayo imeongezeka katika kipindi hiki cha kuanzia Julai 2020 hadi sasa," alifafanua.

Matta aliwataka wateja wa NMB wenye Mastercard na Masterpass QR, kuendelea kufanya ununuzi wa bidhaa na malipo mengine, ili kujiongezea nafasi za kushinda zawadi, ikiwamo ya kufanya utalii wa ndani.

"Zawadi kuu ni ya utalii Zanzibar, Ngorongoro ama Serengeti, inawapa washindi uhuru wa kuchagua zawadi mbadala kama runinga iliyolipiwa DSTV miezi mitatu, jokofu, laptop, simu (Samsung A70), water dispenser na microwave," alisema.

Joram Mtafya, Ofisa wa Bodi ya michezo ya kubahatisha Tanzania (GBT), aliyesimamia droo hiyo amewatoa shaka wateja kuhusu mchakato unaozalisha washindi wa kampeni hiyo.

# Wanne mbaroni tuhuma kuiba nyaya za TANESCO

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Wilaya ya Kipolisi Makambako mkoani Njombe, linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuiba nyaya za umeme zenye thamani ya Sh. milioni 43.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, nyaya hizo zilipaswa kutumika katika usambazaji wa umeme wa Mradi wa Umeme Vijijini (REA).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema tukio la kuibiwa nyaya hizo liligundulika Desemba 12 mwaka jana majira ya asubuhi katika Kata ya Kichiwa, Tarafa ya Makambako mkoani Njombe.

Kamanda Issah alisema siku hiyo, msimamizi wa mradi wa REA wa kata hiyo, Emmanuel Gerad (35), aligundua gramu sita za nyaya za umeme zenye thamani ya Sh. milioni 43 zimeibwa.

Alisema baada ya kupata taarifa ya tukio hilo, Jeshi la Polisi lilifanya upelelezi na kufanikiwa kuwanasa watuhumiwa hao.

"Tumekamata gari aina ya fuso likiwa limebeba aina tofauti ya nyanya za umeme ambazo zinatumika kwenye umeme wa REA," alisema Kamanda Issah.

Kamanda Issah aliongeza: "Katika ufuatiliaji wa tukio hili tumebaini kuna gari iliyohusika kwa sababu kuna nyaraka zilidondoka ya faini ambayo ilitozwa hili gari, matokeo yake hili gari ikajulikana lipo Dar es Salaam na alipofuatwa tajiri wa gari, akasema gari lile lipo mkoani Katavi.

"Tumelikuta Mlele sehemu moja inaitwa Maji Moto, gari lilikamatwa na dereva wake. Baada ya kuwakamata, walikuja kutuonyesha hizi nyaya zikiwa yamehifadhiwa sehemu ya VETA mkoani Mbeya. Kwa hiyo, dereva wa gari aliyefahamika kwa jina la Muhidini Limo amekamatwa."

Kamanda Issah alisema Jeshi la Polisi lipo imara na litahakikisha miradi yote ya serikali inalindwa, hivyo kuwataka wananchi kutoa taarifa kuhusu wanaotaka kukwamisha miradi ya serikali, ili Jeshi la Polisi lichukue hatua stahiki.

HABARI KITAIFA

# Kivuko kipya kuboresha usafiri Chato

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) imeendelea kuboresha huduma za usafiri wa majini nchini baada ya kupokea kivuko kipya cha MV Chato II Hapa Kazi Tu kilichokamilika ujenzi.

Kivuko hicho kimegharimu Sh. bilioni 3.1, kimejengwa na kampuni ya kizalendo ya Songoro Marine Transport Boatyard ya jijini Mwanza na kitakuwa kikitoa huduma kati ya Chato Muharamba na Nkome mkoani Geita.

Akizungumza wakati wa sherehe fupi ya kupokea kivuko hicho jana katika eneo la maegesho ya kivuko, maarufu kama ufukwe wa Chato Mtaa wa Kalema,mkoani Geita, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, aliipongeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na TEMESA kwa kusimamia vyema ujenzi wa kivuko hicho hadi kukamilika.

Aliitaka wizara kuendeleza utaratibu wa kujenga vivuko kwa kutumia makandarasi wa ndani ambao unawawezesha kupata huduma kwa urahisi na kuongeza teknolojia na ajira kwa Watanzania.

Dk. Chamuriho alisema ana imani kuwa kupitia mradi huo wa ujenzi wa kivuko ambao umefanywa na kampuni ya kizalendo, Watanzania waliohusishwa katika ujenzi huo watakuwa wamejifunza teknolojia ya ujenzi wa vivuko na kwa kipato walichokipata wataboresha hali za maisha yao.

Awali, Mtendaji Mkuu wa TEMESA Mhandisi Japhet Maselle, akisoma taarifa fupi ya ujenzi wa kivuko hicho, alisema kivuko cha MV. Chato II kimejengwa kwa mfano wa meli (Landcraft) na sababu ya kujengwa kwa mfumo huo ni kuzingatia mahitaji ya aina ya huduma itakayotolewa na kivuko hicho.

"Tunatarajia mizigo mingi itaongezeka kutoka na kuingia Chato kupitia Muharamba, Senga, Bukondo na Nkome, hivyo ujenzi wa kivuko hiki utakuwa ni chachu kubwa kwa wananchi wa Chato na maeneo ya jirani kuongeza na kukuza uchumi wao hasa kwa wenye kipato cha chini, aidha ni lengo la serikali kutoa usafiri wa uhakika na salama kwa wananchi popote panapohitajika," alisema Mhandisi Maselle.

Vilevile, Mbunge wa Jimbo la Chato ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akizungumza katika tukio hilo aliishukuru kufanikisha ujenzi wa kivuko hicho na kuongeza kuwa kitarahisisha shughuli za biashara kwa wafanyabiashara wa maeneo hayo kwa kutoa fursa kwa wafanyabiashara kupeleka samaki na dagaa wao katika masoko ya Senda na nchi jirani ya Congo DRC.

# Mkuu wa wilaya avalia njuga waharibifu wa mazingira

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Saimon Odunga, ameanzisha msako kudhibiti ukataji miti ovyo unaoharibu mazingira na utumiaji wa nyavu zenye matundu madogo zinazoharibu mazalia ya samaki.

**Pamoja na chakula, kilimo kinawasaidia kuwainua kimaisha na kupata maendeleo.**

Akizungumza na gazeti hili, Odunga alisema ameunda kikosi kazi wilayani hapo kinachofanya msako kuanzia Ziwa Victoria, kuwabaini wavuvi wanaojihusisha na uvuvi haramu kwa kutumia nyavu zilizopigwa marufuku zenye matundu madogo.

Alisema msako huo ni endelevu pia kwa wananchi wanaokata miti ovyo kwa ajili ya biashara ya kuchoma mkaa kwenda kuuza ndani ya Wilaya ya Rorya na nje ya wilaya hiyo hali iliyoathiri maeneo mengi ya Rorya.

Odunga alisema Wilaya ya Rorya inategemea mazao ya chakula kutoka Wilaya ya Tarime na kwamba ukataji miti unaathiri mvua kutonyesha na kusababisha ukame.

Aliwataka wananchi kubadilika kwa kupanda miti, kulima mazao ya chakula na ya biashara yakiwamo mahindi, mihogo, migomba, mpunga na alizeti kwa kuiga wenzao wa wilaya ya Tarime ambayo ina chakula kingi kutokana na wananchi wake kujituma katika kilimo.

Alisema pamoja na chakula, kilimo kinawasaidia kuwainua kimaisha na kupata maendeleo.

Mkuu wa wilaya alisema msako wa wanaokata miti unawahusisha wenyeviti wa vitongoji, vijiji, watendaji wa vijiji na kata na makatibu tarafa kwa kushirikiana na watumishi wa idara za maliasili, misitu na uvuvi.

Aliagiza wanaokamatwa na mkaa wa biashara bila vibali wafikishwe kwenye vyombo vya sheria ili iwe fundisho kwa watu wengine.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari (katikati) akiwa pamoja na walimu na washiriki, baada ya kufungua rasmi awamu ya kwanza ya mafunzo ya ndege zisizo na rubani maarufu ndege nyuki (drone), mafunzo hayo yanatolewa na Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) kinachomilikiwa na TCAA kwa ushirikiano na Chuo cha Pro Wings kutoka Afrika ya Kusini, yanafanyika kwa muda wa wiki nne (moja darasani , tatu mafunzo kwa vitendo). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dampo la kisasa kuboresha mazingira

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Selemani Jafo, amewataka viongozi kusimamia matumizi sahihi ya dampo ili uchafu wote wa Jiji la Mwanza upelekwe eneo hilo.

Akizungumza wakati akikagua ujenzi wa dampo la kisasa lenye ukubwa wa hekta 33.81, eneo la Buhongwa, umbali wa kilomita 16 kutoka jiji hilo, alisema mitambo iliyopo ni gharama na kuwataka kusimamia matumizi sahihi ya mitambo.

Alisema suala la baadhi ya wananchi wanaokusanya chupa katika maeneo hayo lisihusishwe na uharibifu wa miundombinu na matumizi sahihi yazingatiwe kwa kuwa ahitaji maigizo.

"Mmefanya kazi nzuri lazima niwapongeze, lakini msichoke kutembelea wengine kujifunza," alisema Jafo.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira wa Jiji la Mwanza, Danford Kamenya, akiwasilisha taarifa ya usimamizi wa usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu ndani ya dampo hilo, alisema kiwango cha uondoshaji taka ngumu kutoka kwa wazalishaji na kusafirisha hadi kwenye dampo hilo kimeongezeka kutoka tani 238 sawa na asilimia 67 hadi kufikia tani 265 sawa na asilimia 74 kwa siku.

Alisema halmashauri imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuimarisha shughuli za usafi na uhifadhi wa mazingira kwa kushirikisha kampuni binafsi sita na vikundi vya kijamii vitatu ili kutoa huduma za usafishaji wa mazingira katika maeneo yote ya jiji kwa kukusanya, kuzoa na kusafirisha taka ngumu kutoka kwenye vituo 22 na kuhamasisha jamii kushiriki katika kampeni endelevu ya usafi wa mazingira.

Pia, Waziri Jafo alitembelea mradi wa ujenzi wa stendi mpya ya mabasi na maegesho ya malori iliyopo Nyamhongolo na mradi wa ujenzi wa jengo kuu la abiria la uwanja wa ndege jijini humo.

# Waziri Jafo afurahishwa ujenzi wa hospitali

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Selemani Jafo, apongeza ujenzi unaoendelea wa Hospitali ya Wilaya ya Misungwi na kutoa ahadi ya kumshawishi rais ili azidi kuongeza fedha.

Akizungumza wakati akikagua ujenzi huo utaogharimu Sh. 2,076,468,848.00 unaoujumuisha jengo la utawala, wodi ya wazazi, jengo la mionzi, wagonjwa wa nje (OPD), maabara, jengo la kufulia na mashimo ya majitaka mfumo wa TEHAMA, zaidi ya Sh. 462,855 watanufaika na huduma zitakazotolewa.

Alisema kazi iliyosimamiwa na viongozi na watendaji imesimamiwa vyema kukamilika kwa jengo hilo kutawanufaisha wakazi hao.

**Jengo ni zuri na kazi imefanyika ipasavyo nilichokiona hapa kinaushirikiano kuna majengo haya yanavutia kuna watu wengine watajiongopea wanaumwa ili waletwe hapa.**

"Jengo ni zuri na kazi imefanyika ipasavyo nilichokiona hapa kinaushirikiano kuna majengo haya yanavutia kuna watu wengine watajiongopea wanaumwa ili waletwe hapa," alisema Jafo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema watasimamia utekelezaji wa ilani, maendeleo yote hasa miradi inayogusa wananchi na maelekezo yote yaliyotolewa kwa ufanisi.

Akitoa taarifa ya ujenzi huo, Kaimu Mganga Mkuu Wilaya ya Misungwi, Raymond Nyasebwa, alisema ujenzi wa hospitali hiyo umelenga kuimarisha na kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa wilaya hiyo na za jirani, kwa mwaka wa fedha 2019 hadi 2020 walipokea fedha kutoa serikali kuu Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi huo.

Alisema utekelezaji wa ujenzi wa majengo mawili maabara na jengo la OPD ulianza Juni 11, mwaka jana, pia halmashauri inatekeleza ujenzi huo kwa kutumia njia ya 'Force akaunti' na wananchi 156 wamenufaika kwa kupata ajira ya muda mfupi na kuwaongezea kipato chao na kupunguza umaskini.

Akielezea matatizo mbalimbali yanayowasibu, alisema upungufu wa watumishi katika idara ya afya na kwa sasa mahitaji ni watumishi 1,109, waliopo 473 huku pungufu ikiwa ni 636.

Alisema halmashauri hiyo inategemea kuanza kutoa huduma Februari, mwaka huu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi (kulia), wakifungua pazia kuzindua vyumba 11 vya madarasa vilivyojengwa na kukarabatiwa na Benki ya TPB kwa gharama ya Sh. milioni 164 katika Shule ya Msingi ya Nandagala, wilayani Ruangwa, mkoani humo hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ashauri vituo vya afya kusimamia vyanzo mapato

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAGANGA wafawidhi vituo vya afya nchini wametakiwa kusimamia vyanzo vya mapato katika maeneo yao ya kazi kuhakikisha huduma za afya zinazidi kuboreshwa.

Hayo yalisemwa na Dk. Festo Diganga, ambaye ni Naibu kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, kitengo cha afya na miundombinu, wakati alipofanya ziara katika Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani kukagua huduma za afya na miundombinu ya barabara.

"Kila kituo cha afya kihakikishe kinasimamia vyanzo vya mapato ili kusaidia upatikanaji wa huduma bora za kiafya," alisema.

Alisema vyanzo vya mapato vinatakiwa visimamiwe hali itakayosaidia kufuata mwongozo ambao unataka asilimia 67 inunue dawa.

Alisema vituo vya afya vikisimamia vizuri vyanzo vya mapato vitaacha kuwa tegemezi na usimamizi wa mapato utawasaidia kununua vifungashio, dawa na vifaa tiba na kupunguza kupewa dawa na Bohari ya Dawa (MSD).

Alitaka mifuko ya NHIF isimamiwe vizuri ili wananchi wawe na imani nao.

"Wapo watu wasio waaminifu wanaochukua pesa za wanachama na kushindwa kuzipeleka benki kwa wakati hali inayochangia usumbufu," alisema.

Alisema katika taarifa za afya za Mkuranga alizopewa alibaini kuwapo na kasoro ambazo inatakiwa zifanyiwe kazi.

Alisema kwa kipindi cha miezi sita haijailipa Mkuranga malipo yao na cha kushangaza hakuna hatua zilizochukuliwa.

Alisema kuwa huduma mbovu zinatolewa kwa wagonjwa wenye kadi za CHF zimekuwa na malalamiko kutoka kwa wagonjwa na kudai hata baadhi ya dawa na vipimo kutopatikana.

Vile vile, alisema kinachotakiwa ni jamii kuelimishwa kuhusu mifuko hiyo ili waweze kujiunga na kunufaika nayo.

Pia Naibu Waziri huyo aliuagiza uongozi wa Hospitali ya Mkuranga kusimamia vyanzo vya mapato ili kuleta maendeleo.

## Madiwani wajadili upungufu wa madarasa

**Na Timothy Itembe,** MARA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Tarime DC mkoani Mara, limejadili ukamilishaji wa upungufu wa vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari na msingi.

Ripoti ya Mkurugenzi, Apoll Tindwa mbele ya baraza ilisema kuwa kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 16 ili kukamilisha malengo.

Taarifa hiyo ilisema kuwa wanafunzi 6,265 wakiwamo wasichana 4,098 na wavulana 3,227 sawa na asilimia 79.4 walifanya mtihani wa kuingia kidato cha kwanza kwa mwaka 2020/2021.

Mkurugenzi huyo aliomba kupatiwa fedha kutoka Mfuko wa Jamii (CSR), Sh. 656,160,000 kwa lengo la ukamilishaji wa miundombinu na samani za shule ili ifikapo Januari 11, 2021, watoto wakaanze masomo.

Hata hivyo, kwa upande wa Halmashauri ya Tarime Mjini kupitia diwani wake, Chacha Marwa Machugu, alimpongeza Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Elias Ntiruhungwa kuwaunga mkono na kutoa mabati 432.

Machungu alisema mabati hayo yanaenda kukamilisha vyumba saba vya madarasa pamoja na nyumba moja ya utawala ili wanafunzi waanze masomo Januari 11.

"Mimi nampongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime Mjini, Elias Ntiruhungwa, kutoa sapoti ya mabati ya ukamilishaji wa madarasa na pia shukrani hizo ziende kwa Rais John Magufuli, kuhimiza watendaji kusimamia madarasa na shukurani hizo ziwaendee wadau wote wa maendeleo waliotuunga mkono pamoja na wazazi wa watoto waliochangia shughuli mbalimbali ikwamo kutoa fedha za mfukoni, wananchi kwa ujumla ambao walituunga mkono na kuumwa na uchungu wa elimu," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya Tarime, Mtemi Msafiri, aliwataka madiwani pamoja na watumishi kwa ujumla kutoa ushirikiano wa dhati ili kuhakikisha wanafunzi wanaenda kuanza masomo.

**Mabati hayo yanaenda kukamilisha vyumba saba vya madarasa pamoja na nyumba moja ya utawala ili wanafunzi waanze masomo Januari 11.**

Membe anapodhihirisha siasa si uadui

Ukurasa 13





Ukurasa 14

## URSULA VON DER LEYEN

## Mwana mama anayeuongoza Umoja Ulaya

siasa

JUMATANO JANUARI 6, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# KATIBU MKUU ZENA AHMED SAID

- ‘Mwanajeshi kubwa’ wa 1 tangu mapinduzi 1964
- Kutoka KM Nishati hadi Katibu Mkuu Kiongozi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NI kwa mara ya kwanza baada ya miaka 57 ya uhuru wa Zanzibar inaongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi mwanamama, Zena Ahmed Said, anayevunja rekodi na ambaye pamoja na wadhifa huo anakuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi.

Februari mwaka jana Rais John Magufuli, alimteua kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, akichukua nafasi ya Dk. Hamisi Mwinyimvua aliyestaafu, leo anaongea habari nyingine, ni baada ya kuwa na jukumu kubwa zaidi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Uteuzi wake unachukuliwa kuwa ni utekelezaji wa ahadi za Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyoitoa kwa wanawake kuwa endapo atapata ridhaa ya kuwa Rais atawapa kipaumbele kwa kuwateua kushika nafasi mbalimbali serikalini.

Akizungumza baada ya kutangaza Baraza la Mawaziri Rais Mwinyi, anasema katika nafasi atakazoteua, hatakuwa na ubaguzi wa kijinsia, hivyo atamteua yeyote kulingana na vigezo kuanzia elimu, ubunifu na utendaji kazi wa kimaadili bila ya kujali jinsia.

Kumtangaza Zena kuwa Katibu Mkuu Kiongozi nafasi ambayo kwa miaka yote ilishikiliwa na wanaume, kumeshangiliwa na kufurahiwa na wanaharakati wa kutetea maendeleo, haki za watoto na wanawake.



Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmed Said, akila kiapo mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### UTEUZI WA ZENA

Baada ya kula kiapo cha utii na uaminifu, Katibu Mkuu Kiongozi Zena, anaahidi kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kufikia matarajio ya Wazanzibari.

“Nitafuata kanuni na sheria na kujiongeza katika ubunifu ili kufikia malengo, na kuangalia kwa undani suala la ajira kwa vijana ili kulipatia ufumbuzi,” anaahidi.

Anawatolea wito wanawake kujiamini na kufanya kazi zao kwa weledi pamoja na kuzingatia muda na nafasi zao, lakini wasisubiri kusaidiwa au kudhani kuwa watawezeshwa.

Kabla ya uteuzi huo, Zena ambaye kitaaluma ni mhandisi alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Tanzania Bara, anasema wakati unapofanyakazi ukiwa na hofu, hutafanikiwa hivyo hataipa nafasi na kuahidi kutekeleza majukumu yake vizuri kwa wakati na kwa viwango stahiki.

Anaongeza: “Wakati unafanyakazi ukiwa na hofu ya kuwa ni mwanamke utashindwa, woga utakuangusha kwenye nafasi yoyote unayopewa ifanye kwa weledi wa hali ya juu acha matendo yako na kazi zako zionekane zenyewe.”

Anakumbusha kuwa unapotenda kazi vizuri, utaaminiwa bila ya kujali jinsia, hivyo anawataka wanawake kufanya kazi bila hofu na utendaji wao uwazungumzie wala si kujisifu au kujigamba.

Anasema, wanawake wana majukumu mengi ikiwamo ya familia hivyo waangalie majukumu yao kwa wakati stahiki ili kazi ziende vizuri na wakifanya kazi kwa weledi, wataaminiwa bila ya kujali jinsia.

“Tunapopewa nafasi wanawake tuzitumikie kikamilifu lakini tusikwepe majukumu yetu katika familia, nikiwa katika familia yangu nafasi ya uongozi serikalini naiweka pembeni namtii mume wangu na kushughulikia familia kama inavyotakiwa,” Katibu Mkuu Kiongozi.

Licha ya kuunda Baraza la Mawaziri lenye wanawake wanne kati ya mawaziri 13 aliowateua hivi, Rais Mwinyi, aliteua pia wakuu wa wilaya wanne kati ya 11 wakati Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba pia ni mwanamama.

### MAWAZIRI WASHANGILIA

Mawaziri wanawake wa Zanzibar wamsema kuwa wanawake ni jeshi kubwa katika kuleta maendeleo, hivyo wanampongeza Rais kwa kuwapa kipaumbele na kuwachagulia mwanajeshi Zena kuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lema Muhamed Mussa, anasema mwanamke ana nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko ya maendeleo kuliko mwanaume.

“Unapomwelimisha mwanamke umeelimisha jamii tofauti na mwanaume anapoelimika ni yeye peke yake, hivyo kuteuliwa injinia Zena, kinatupa ari sisi wanawake na kutarajia kuona kasi mpya ya maendeleo na mabadiliko yatakuwa makubwa.”

Waziri wa Habari, Vijina na Michezo, Tabia Mwita, anasema uteuzi huo ameupokea kwa furaha na kwamba Rais Mwinyi anazidi kujenga imani kwa wananchi kwa sababu anatekeleza yale ambayo aliwaahidi ikiwemo kuwapa nafasi kinamama.

Kwa upande wake Waziri wa Ardhi na Makazi, Riziki Juma Pembe, anaupokea uteuzi huo kwa furaha akisema amefarijika kuona jinsi Rais, anavyowaamini wanawake na sasa Katibu Mkuu Kiongozi, atalithibitisha hilo kuwa ni mtendaji chapakazi hodari hivyo kazi zitakwenda sawasawa.

### TAMWA YAKUNWA

Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), upande wa Zanzibar kimefurahishwa na uteuzi wa Katibu Mkuu Kiongozi na kupongeza ujasiri wa Rais Mwinyo kuwaamini wanawake katika uongozi.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, anasema kuwapa kipaumbele wanawake hasa katika nafasi hiyo ambayo haijawahi kushikiliwa na mwanamke ni jambo la kihistoria.

“Nimefurahi sana kwa sababu nafasi hiyo anahitaji mtu mwenye uwezo wa kuangalia bila ya ubaguzi na Zena kwa kuwa ni mkuu wa utumishi tunaamini kuwa ataweka mifumo bora ya ajira kwa mujibu wa mtumishi na taaluma yake na si kwa ujamaa.

Naamini atawezesha idara ya utumishi kupata mabadiliko makubwa na endelevu,” anasema Dk. Mzuri.

Anasema, ni matumaini yake kuwa kiongozi huyo ataleta nidhamu ya hali ya juu kiutendaji ili ripoti za serikali ziwe zinapatikana kwa wakati na usimamizi wa kazi za umma ufanyike kwa weledi, kimaadili na kutumikia wananchi ambao ndiyo msingi mkuu wa mamlaka.

Anawakumbusha wanawake kuwa wana uwezo mkubwa, hivyo hilo litathibitika kwa kuwa Zena ataleta mabadiliko chanya serikalini hasa ikizingatiwa ni msomi, mweledi na mbunifu.

“TAMWA moja ya kilio chetu ni nafasi za uongozi kwa wanawake hivyo ule msemo wa Rais Dk. Mwinyi usemao kuwa yajayo yanafurahisha, kweli tumeanza kufurahi, tunamuomba aendelee kuwaamini wanawake kwa sababu ni watu hodari katika utendaji wa kazi na waaminifu,” anasema Mzuri.

Anawataka wanawake na wote waliopewa nafasi ya uongozi kuwajibika na kuendana na kasi ya Rais Mwinyi ya kuwaletea maendeleo wananchi kwa vile kiu ya kila mmoja na kuona Wazanzibari wanakuwa na maisha bora na kuondokana na umaskini.

## GEORGE MKUCHIKA:

# Mkongwe aliyedumu serikalini awamu zote



**Na Ani Jozeni**

MMOJA wa mawaziri wakongwe wanaodumu katika Baraza la Mawaziri kwa takribani miongo minne sasa ni George Mkuchika (pichani), wakati huu akikabidhiwa tena mikoba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Manejimenti na Umma na Utawala Bora katika serikali ya awamu ya tano, kazi aliyoianza tangu awamu ya nne.

Baadhi ya taarifa japo ni kwa kifupi na hazina maelezo ya kutosha, zinaonyesha kuwa kepteni mstaafu Mkuchika amekuwa serikalini kuanzia awamu ya tatu kama mkuu wa mkoa wa Tanga kuanzia mwaka 1997 hadi 2005 ambako alichaguliwa kuwa Mbunge wa Newala.

Zinaonyesha kuwa aliingia kwenye Baraza la Mawaziri Februari 2008 kama Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo hadi Novemba 2010.

Baada ya hapo alirejea tena katika Baraza la Mawaziri akiwa Ofisi ya Rais TAMISEMI -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kuondoka katika mabadiliko ya Mei 2012 akarudi tena Oktoba 2017.

Taarifa hizo zinaonyesha kuwa waziri huyo amekuwa akifanya kazi za kisiasa tangu 1997 na kwa wanaomfahamu au kukumbuka jina la George Mkuchika wanafahamu kuwa ana mengi katika uongozi wa nchi.

Alikuwa mkuu wa mkoa kazi inayofanywa kwa mzunguko kwenye nafasi za uongozi baada ya kutumikia katika ngazi za juu.

Kuna kawaida kuwa mbunge akishindwa kura katika kutetea kiti chake na serikali bado inamhitaji kwenye utumishi wake, anapata nafasi hasa ya kuwa mkuu wa wilaya, wakati waziri kwa kawaida alikuwa anapewa nafasi ya mkuu wa mkoa, aendelee kutumikia serikali kutokana na uzoefu na utii alionao.

Kwa kifupi unaweza kusema Mkuchika aliyezaliwa 1948 yupo serikalini kwa miaka zaidi ya 40.

Wasifu wa mtandao unaonyesha amehitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, bila maelezo ya kina ya vipindi vyake vya masomo na kazi hadi kufikia mwaka 1997.

> Kuna kawaida kuwa mbunge akishindwa kura katika kutetea kiti chake na serikali bado inamhitaji kwenye utumishi wake, anapata nafasi hasa ya kuwa mkuu wa wilaya, wakati waziri kwa kawaida alikuwa anapewa nafasi ya mkuu wa mkoa, aendelee kutumikia serikali kutokana na uzoefu na utii alionao.

Wanaofuatilia taarifa zake wanapata picha kuwa ndipo alianza kutambuliwa na wakuu serikalini akawa mkuu wa mkoa. Kiongozi huyo ni mkongwe aliyeanza safari yake ya pili ya utumishi serikalini muda mrefu na akapitia tena kote alikopita mapema.

Wako wanaoshangaa kwanini watawala waandamizi serikalini hawapati viongozi wengine katika nafasi kama hizo, na kuendelea kutegemea wale ambao wamekuwapo huko miaka yote.

Mwingine mwenye nafasi kama ya kapteni mstaafu Mkuchika ni Mzee Philip Mangula, Makamu Mwenyekitii wa Chama Cha Mapinduzi (Bara) ambaye ameendelea katika nafasi hiyo, huku viongozi vijana zaidi yake katika chama waking'atuka.

Ni nafasi ambayo kwa kawaida inahitaji mtu mwenye wadhifa wa Katibu Mkuu wa CCM au Waziri Mkuu wa Tanzania kuishika, kwani marais walipita hawawezi kuikamata.

Ukiangalia nafasi ya kapteni mstaafu Mkuchika katika utawala bora unaweza kumfananisha na jinsi alivyoingia Hayati Kingunge Ngombale-Mwitu kama Waziri wa TAMISEMI mwaka 1995 baada ya Frederick Sumaye kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu.

Wachunguzi wa masuala ya siasa wakati ule, baadhi yao waliona kuna umuhimu kwa Rais Benjamin Mkapa, kuteua waziri mwenye uzoefu na hata ukomavu katika eneo hilo, kwani bila kuifahamu mikoa kiutendaji kwa muda mrefu, anayepewa nafasi hiyo (au waziri mkuu) anaweza kuelemewa hata na majungu akakwama.

Sumaye alikuwa wakati huo ana historia au uzoefu wa uwaziri kamili akiwa ni Wizara wa Kilimo, kwa takriban miezi sita kabla ya bunge kuvunjwa ili kwenda kwenye kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 1995, hivyo hakuwa mzoefu wa mikoa.

Baadhi ya wazoefu wa uchambuzi walihisi kuwa anahitajika waziri katika nafasi hiyo mwenye uzoefu wa kutosha, kuhusiana na kilichokuwa kinaendelea katika kila mkoa katika masuala ya maendeleo kwa miaka iliyotangulia.

Uelewa huo katika mazingira ya nchi ni pamoja na kujua hali ya chama katika mkoa fulani, kwa mfano migongano ya kimaslahi na madai ya maeneo tofauti, kwa mfano wilaya, kwa serikali, na nini kinachoendelea katika mahusiano kati ya wenyeji wa mikoa hiyo na wawakilishi wa serikali kuu, yaani wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya.

Akateuliwa hayati Ngombale-Mwiru amsaidie waziri mkuu kwenye eneo hilo.

Inapokuja hali hii ya kuwepo waziri mzoefu na mbobezi serikalini, kwa nafasi ya utawala bora, ni wazi kuwa ipo kazi eneo hilo inayofanana na ile ya TAMISEMI.

Ukiangalia kwa karibu unakuta serikali ya awamu ya tano imefanya kazi kubwa kuvunja ngome za ubadhirifu na uonevu, upendeleo, ubabaishaji na usultani wa kujuana, kutokana na matumizi ya vyeti feki na kuwapo kwa maelfu ya wafanyakazi hewa.

Ilitakiwa awepo mtu wa kusimamia zoezi hilo ambaye 'akimuua nyani, hamwangalii machoni,' asijikwae kwa kile alichotumwa kufanya.

Kwa lugha ya Mwongozo wa TANU wa 1971 alikuwa kada mzalendo, 'asiye na inda, wala waa...' mwenye dhamira halisi kukalimisha mabadiliko ya msingi ya serikali iliyopo sasa.

Ndiyo maana kuna mijadala ya uandishi wa historia ambayo kwa kawaida inaegemea zaidi wale wakuu, kwa mfano Julius Caesar na kuinuliwa kwa himaya ya Warumi, au Julius Mwalimu Nyerere na kujengwa TANU, uimarishaji wa dola ya aina fulani hapa nchini. Ndiye kiongozi lakini kuna wengi waliofanya kazi za kutukuka kuwezesha azma hiyo ifanikiwe ambao hata wakati wa maisha yao huwa wanajulikana kwa uchache tu. Mara nyingine wakifikia tamati ya maisha baadhi ya walioyafanya yanakumbukwa, ila uzoefu unaonyesha kuwa sifa zao zinaenea ukizungumza na waliowafahamu, hivyo kupungua hatua kwa hatua.

# Membe anapodhihirisha siasa si uadui

## •Akwepa malumbano na ACT-Wazalendo
## •Lakini hajasema kama nyumbani kumenoga



Bernard Membe

**Na Sabato Kasika**

KUHAMA chama na kwenda kingine si kosa kwa vile kikatiba ni haki ya raia na pia zipo sababu mojawapo ni kuvutiwa na sera, malengo, falsafa na itikadi zake na inawezekana wanapopakimbia vyote havipo.

Katika makundi hayo ya kuhama vyama, wapo wanaohama kwa sababu ya kukimbia migogoro, wanaokwenda kutafuta nyadhifa, wengine ni wasaka tonge hasa fedha na fursa kiuchumi.

Lakini katika siasa, wapo wanaoamua kujiondoa kwenye vyama na kukaa pembeni, kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kupumzika siasa au kwa sababu wanaona mambo katika chama chao yanakwenda 'segemnege' au kombo.

Mbaya zaidi miongoni mwao wapo wanaoponda viongozi wakuu wa vyama vyao vya awali, kuvishushia tuhuma na kutumia siasa za majitaka kuwapaka wakuu hao kila wakati. Kwao nyingi ni lawama na kila aina ya kejeli, hali inayoonyesha kuwa hawana ukomavu wa kisiasa.

Wanaofanya mambo ya aina hiyo, wanasahau kwamba, siasa si uadui au malumbano yasiyo na tija bali inakwenda sambamba uvumilivu unaotokana na ukomavu na kuaminiana kwenye harakati za ujenzi demokrasia na siasa zenye maoni na mitizamo tofauti.

Ikumbukwe kuwa chuki za kisiasa, kukomoana na malumbano yasiyo na mwisho, mara nyingi havileti afya kwa chama au hata wanachama, katika maendeleo ya demokrasia, badala yake ukomavu wa kisiasa unatakiwa kumiliki na kutawala.

Huo ndiyo msingi wa kuepusha hayo yote ambayo huambatana na siasa za majitaka na kusababisha baadhi ya wanasiasa kuchukiana hata kwa mambo ambayo wangeweza kuyamaliza kimya kimya.

**UKOMAVU WA CHAMA**

Aliyekuwa mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha ACT- Wazalendo, Bernard Membe, ameamua kuachana na chama hicho alichojiunga nacho miezi mitano na nusu iliyopita.

Tofauti na baadhi ya vyama, ambavyo kuondoka kwa wanachama au mwanachama wake huzusha malumbano na kurushiana hili na lile, ACT-Wazalendo pamoja na mwanachama wake huyo hawakuyapa nafasi hayo.

Katika mahojiano yake na gazeti hili juzi, Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, anasema, hawana nafasi ya kujiingiza katika malumbano na mwanasiasa huyo aliyetokea CCM na kuwa mwanachama wao, ambaye alipewa wadhifa wa kugombea urais wa Tanzania kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

> "Taarifa za Membe kujiuzulu uanachama na kujivua nafasi zote za uongozi tumezipokea, na kimsingi siyo taarifa ngeni, kwa sababu tumekuwa tukizifahamu. Membe mwenyewe amewasiliana na sisi mara kadhaa, chama hakitajiingiza katika malumbano na mwanasiasa huyo," anasema Shaibu.

Shaibu anasema, chama chao kilikuwa na taarifa za kusudio hilo la Membe kwa muda mrefu, kwamba, hata baada ya uchaguzi mkuu, ilikuwa ni kana kwamba ameshajiweka pembeni na shughuli za chama.

"Taarifa za Membe kujiuzulu uanachama na kujivua nafasi zote za uongozi tumezipokea, na kimsingi siyo taarifa ngeni, kwa sababu tumekuwa tukizifahamu. Membe mwenyewe amewasiliana na sisi mara kadhaa, chama hakitajiingiza katika malumbano na mwanasiasa huyo," anasema Shaibu.

Katibu huyo anasema, ACT-Wazalendo wana utamaduni wa muda mrefu na kwamba mtu yeyote akijiondosha kwenye chama, mara nyingi wanajiepusha na malumbano na wanamtakia mkongwe huyo wa siasa kila la heri.

Majibu hayo yanaonyesha ni jinsi gani viongozi wa chama hicho wamekomaa kisiasa hasa baada ya kuondoka kwa mwanachama wake, lakini kinakataa kuanza malumbano naye.

**MSIMAMO WA MEMBE**

Desemba mosi mwaka huu akiwa kijijini kwake, Rondo Chiponda mkoani Lindi, mwanasiasa huyo anasema; "Ibara ya 105 ya kifungu kidogo cha kwanza cha katiba ya ACT-Wazalendo, inasema, mwanachama atakoma kuwa mwanachama na atajiuzulu iwapo atatangaza kuwa amejiuzulu au ataandika barua kwa viongozi wa chama, na mimi nimefanya yote mawili," anasema Membe.

Katika maelezo yake kwa vyombo vya habari, anasema, hakulazimishwa na mtu yeyote, bali ni uamuzi wake binafsi na kwamba, anatumia haki yake ya kikatiba ya kujiuzulu nafasi yake ya ushauri mkuu wa chama na uanachama.

Hata hivyo, tofauti na baadhi ya wanasiasa, ambao huhama vyama vyao na kuanza kurusha lawama na tuhuma kule wanakotoka, Membe hakufanya hivyo, badala yake anaeleza hatua halali alizochukua kujiweka pembeni.

Maelezo ya mwanasiasa huyo na wa viongozi wa kule alikotoka, yanaonyesha wazi kuwa wote wamekaa timamu kisiasa, kwa kuwa hakuna malumbano ama kulaumiana au kushutumiana kwa aina yoyote.

Kwa jinsi alivyojiengua, anaweza kuwa fundisho kwa baadhi ya wanasiasa wasio na uvumilivu wa kisiasa, kwa kuwa hakulaumu CCM wakati anahamia ACT-Wazalendo na pia hakulaumu chama hicho wakati anajiondoa.

Mwanasiasa huyo amejitoa kwenye chama chake ACT- Wazalendo ambacho amedumu nacho kama miezi mitano na nusu, huku akielekeza kuwa amefanya hivyo akiwa ametimiza matakwa ya katiba ya chama hicho.

**ALIVYOANZA SAFARI**

Ilikuwa ni Februari 28 mwaka jana, CCM ilimvua uanachama, kwa tuhuma za kukiuka maadili ya chama hicho, kwamba mwenendo wake haukuwa mzuri, na kwamba tangu alipobadilika alisaidiwa lakini hakujirekebisha.

Hiyo ilikuwa ni taarifa ya Katibu Mwenezi wa CCM, Humphrey Polepole, wakati akitangaza kumwondoa katika chama, huku makatibu wakuu wa zamani wa CCM, Yusuf Makamba na Abdulrahman Kinana nao wakiguswa.

Makamba alisamehewa, lakini Kinana alionywa kwa karipio, na kuanzia hapo, Membe hakuwa mwanachama wa CCM, kisha baadaye akaibukia katika Chama cha ACT-Wazalendo.

Julai 16 mwaka jana alitua katika chama hicho na kisha baadaye akapitishwa kuwania nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu uliopita na kuzindulia kampeni zake mkoani Lindi, lakini baada ya jukumu hilo hakuonekana tena katika majukwaa ya kampeni hizo, hadi uchaguzi kufanyika bila yeye kusikika kama mwanzoni, hatimaye ameamua kujiondoka rasmi ndani ya ACT-Wazalendo.

Licha ya kwamba kulikuwa na hisia kuwa kama walivyofanya Mawaziri Wakuu wa zamani, Edward Lowassa na Frederick Sumaye kurudi CCM, Membe naye alitarajiwa atafuata nyayo zao.

Lakini wakati wa kampeni aliulizwa kuwa nawe si mmoja wao? Alijibu kuwa yeye tofauti na hao, alifukuzwa, hata hivyo kujiondoa kwake kunaendelea kutafsiriwa kuwa pengine ni maandilizi ya kurejea katika chama chake cha mwanzo.

## JUKWAA LA UONGOZI



### URSULA VON DER LEYEN

# Mwana mama anayeuongoza Umoja Ulaya

**Na Mwandishi Wetu**

"KWANGU ni kama nimerudi nyumbani," anasema Ursula von der Leyen, wakati akipokea jukumu la kuwa Rais wa Tume ya Umoja wa Ulaya. Ni kwa mujibu wa makala ya BBC iliyoandikwa Desemba 11, 2020.

Akiwa mzaliwa na mkulia wa jijini Brussels nchini Ubelgiji ambayo ni makao makuu ya Umoja wa Ulaya (EU) Waziri wa zamani wa Ulinzi wa Ujerumani wakati wa uongozi wa Chansela Angela Merkel, ni shupavu na mwanamke wa kwanza kuuongoza umoja huo.

Anasema ni kama amerudi nyumbani kwa sababu ni kizazi cha vigogo wa Umoja wa Ulaya maana tangu awali baba yake alikuwa miongoni mwa makamishna wa chombo hicho kikongwe duniani cha kisiasa na kiuchumi.

**ALIKOTOKA**

Ursula von der Leyen alizaliwa Brussels mwaka 1958, na kusoma kozi mbalimbali kuanzia lugha, uchumi na nyinginezo na kwamba baba yake ni miongoni mwa maofisa walioiongoza iliyokuwa Jumuiya ya Uchumi wa Nchi za Ulaya (European Economic Community -EEC) kabla ya kuwa EU.

Baba wa Ursula von der Leyen, Ernst Albrecht, alikuwa kamishna mwandamizi wa EEC jijini Brussels miaka ya 1950 kabla ya kujiingiza kwenye siasa za Ujerumani akiwa mwanachama wa Chama cha Wahafidhina cha Christian Democrats (CDU), ambacho leo kinaongoza nchi hiyo kikiongozwa na Chansela Merkel.

Ursula von der Leyen, alichukua nafasi ya Jean-Claude Juncker , aliyemwachia kijiti hicho Desemba 1, 2019, alianza na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Uingereza inaondoka EU kupitia mpango wa Brexit 'British Exit '.

Alipochaguliwa mataifa mengi-

> "Mtangulizi wake Junker aliandika kwenye ukurasa wake wa 'twita' kwamba wadhifa wa Rais wa Halmashauri Kuu ni nafasi yenye wajibu mzito na kuelezea imani yake kwamba Von der Leyen anayekuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo atakuwa kiongozi wa aina yake.

wanachama wa EU walipongeza na kumsifu Ursula von Der Leyen kuchaguliwa kushika wadhifa huo akiwa mwanamama wa kwanza kuongoza Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya.

Kansela Angela Merkel wa Ujerumani tangu mwanzo amekuwa akimsifu waziri huyo kwenye baraza lake la mawaziri akisema anaamini mwanasiasa huyo kutoka Ujerumani atakabiliana na changamoto za umoja huo kwa ujasiri mkubwa.

Baada ya kura za kumwidhinisha, Von der Leyen alisema "Nimepata ahueni na nina furaha kwa sababu ushindi mwembamba. Nilikuwa na siku 13 pekee kuwashawishi wabunge hapa katika bunge la Ulaya. Na bila shaka walihitaji kufahamu mimi ni nani, ninawaza nini na mpango wangu ni upi.

Na kutimiza hilo ndani ya siku 13 ilikuwa kama mbio ndefu lakini ilistahili kuwa hivyo."

Mtangulizi wake Junker aliandika kwenye ukurasa wake wa 'twita' kwamba wadhifa wa Rais wa Halmashauri Kuu ni nafasi yenye wajibu mzito na kuelezea imani yake kwamba Von der leyen anayekuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo atakuwa kiongozi wa aina yake.

Chini ya wadhifa huo Von der Leyen atakuwa na jukumu la mstari wa mbele la kuweka malengo ya kisiasa ya Umoja wa Ulaya katika kipindi cha miaka mitano ijayo, huko akisimamia zaidi ya wafanyakazi 32,000 wa umoja huo.

Alianza kazi akiwa na majukumu kadhaa mojawapo ni Brexit ambalo sasa amemalizana nalo. Suala jingine ni mabadiliko ya tabianchi na kuahidi kuwa atafanikisha kuwana Ulaya ya Kijani na kuondoa uzalishaji wa hewa za sumu za viwandani zinazochangia ongezeko la joto duniani kabla ya 2050, na kuanzisha mfuko wa nishati kwa mataifa yanayotegemea umeme na nishati ya visukuku.

Kwa upande wa usawa wa kijinsia alichagua timu ya makamishna 27 wa EU wakiwamo wanawake 12 , anaofanya nao kazi pamoja.

Suala jingine ni uhamiaji, aliahidi kuwa atabadilisha mifumo ya EU ya kuomba hifadhi ya kisiasa kwa wageni ambayo wanachama wa umoja huo wamehangaika nayo kwa miongo kadhaa sasa.

Aliahidi kutanua eneo la EU na kupanua matumizi ya visa ya Schengen inayotumiwa na nchi wanachama wa umoja huo na kuwataka wanachama wajiandae kusajili wanachama wapya wa Balkan.

Mataifa ya Balkan pamoja na nchi za Kusini Mashariki mwa Ulaya zikiwamo Macedonia, Bosnia na Herzegovina, Kosovo na Croatia.

Mama Ursula anatamani ulinzi wa pamoja na kuahidi kuwa atakuwa mshiriki wa Umoja wa Kujihami wa Nchi za Atlantiki Kaskazini (NATO) kama mdau muhimu wa masuala ya ulinzi wa pamoja, hivyo wana EU wanatakiwa kuwekeza pamoja.

**VIPORO VYA LAWAMA**

Alipochaguliwa alitajwa kuwa hakuwa chaguo la kwanza, lakini alibahatika kuchukua wadhifa huo baada ya wengine kujitoa kwenye nafasi ya kubeba jukumu hilo.

Wabaya wake wanasema hakuwa na nafasi kubwa, lakini ndiye anayeiongoza Ulaya. Anaelezwa kuwa hakuwa maarufu hata alipokuwa Waziri wa Ulinzi wa Ujerumani lakini alipopendekezwa aliungaa mkono na Bunge la Ulaya.

Mama von der Leyen anasifiwa kuwa ni mchapakazi hodari japo wakati akiwa kwenye ulinzi alituhumiwa kuwa na mikataba na kandarasi za jeshi zenye utata na kuna wakati alidaiwa kuhusika na matumizi mabaya ya fedha kwenye wizara hiyo.

***BBC/DW***



## HABARI DODOMA

# Serikali yajipanga kuleta mapinduzi ya kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imejipanga kuleta mapinduzi ya sekta ya kilimo kwa kuboresha huduma za ugani, ili wakulima waweze kuzalisha kwa tija na kuongeza pato la taifa.

Hatua hiyo itafikiwa kutokana na mipango ya wizara ambayo imeandaa mkutano maalum wa maofisa kilimo wa mikoa na halmashauri nchini kujadili tatizo na suluhisho la upatikanaji wa huduma bora za ugani ili wakulima wapate tija na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Hayo, yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, wakati alipotembelea Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Makutupola.

Prof. Mkenda, alisema mkutano huo utakaofanyika wiki ijayo utahusisha maofisa kilimo wa mikoa na halmashauri zote nchini ili kuweka mikakati itakayoingizwa kwenye bajeti ya wizara ya mwaka.

2021/2022 kuwezesha kutatua kwa hatua, changamoto za huduma za ugani kwa wakulima.

"Tunataka tutenge fedha mahsusi kwenye bajeti ijayo 2021/2022 kwa ajili ya kuboresha huduma za ugani, kwa kuwafundisha maafisa ugani kanuni bora za usimamizi wa mazao ya zabibu, pamba," alisema.

"Kwa kuanzia tutachagua mikoa baadhi ya kuanza utekelezaji ili baada ya mwaka mmoja tupime matokeo yake kwenye uzalishaji na tija," alisema Prof. Mkenda.

Alisema wizara inapitia bajeti ijayo, fedha zitatengwa ili itoe mafunzo kwa maofisa ugani kuhusu mazao ili wayajue na kufundisha kanuni bora kwa wakulima nchini.

"Kwa kweli tunahitaji mapinduzi ya kilimo tunazungumza kilimo ni uti wa mgongo, maneno yametosha, lazima twende kwenye vitendo kuhakikisha tija inaonekana kwenye kilimo, ikiwamo kueneza huduma za kumsaidia mkulima kuongeza uzalishaji," alisema Mkenda.

Alisema Wizara ya Kilimo inathamini shughuli za ugani na itafanya jitihada kuwakutanisha wataalamu hao na kuwajengea uwezo wa kufanya kilimo cha kisayansi na kuachana cha mazoea.

# Aliyeokoa watoto chooni atunukiwa cheti, fedha

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amemkabidhi cheti na fedha taslimu Sh. milioni moja, Koplo Denis Minja wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutokana na kuokoa watoto wawili tofauti ndani ya mwaka mmoja katika mashimo ya vyoo.

Koplo Minja aliokoa watoto hao mwaka jana, waliokuwa wamepata majanga ya kutumbukia kwenye mashimo ya vyoo katika matukio mawili tofauti.

Akizungumza na waandishi wa habari, Simbachawene alisema kitendo alichokifanya koplo Minja ni cha kijasiri na kinahitaji moyo wa kipekee kwa sababu kuingia ndani ya shimo la choo si kazi rahisi.

Alisema askari huyo anastahili kupewa motisha ili kuhamasisha wengine kufanya hivyo.

"Tukio hili lilisambaa maeneo mengi duniani na jamii iliona hivyo kuna haja ya kuwasiliana na wadau kwa ajili ya kupata vifaa vya uokoaji vya mtu mmoja mmoja," alisema Simbachawene.

**Tukio hili lilisambaa maeneo mengi duniani na jamii iliona hivyo kuna haja ya kuwasiliana na wadau kwa ajili ya kupata vifaa vya uokoaji vya mtu mmoja mmoja.**

Alilipongeza jeshi hilo kwa kuwa na vijana wenye ari na nguvu ya uokoajii katika majukumu ambayo wamekabidhiwa.

Simbachawene alisema wanafahamu kuwa kuna matatizo ya vifaa, kutokana na tukio na kuahidi kuzungumza na wadau ili kuagiza vifaa vya uokoaji vya mtu mmoja mmoja.

Katibu Tawala na Fedha wa Jeshi hilo, Mbaraka Semwanza, alisema kitendo cha kumpongeza Koplo Denis kimewafanya maofisa na maaskari wa jeshi hilo kuongeza morali zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema, pamoja na kuwa na tatizo la vifaa, lakini wataendelea kuchapa kazi kulingana na walivyofundishwa huku akimuhakikisha wako tayari kwenda katika matukio yoyote ya majanga ili kuhakikisha jamii inakuwa salama.

Awali, akisoma taarifa fupi ya Koplo Denis kuhusu uokoaji aliofanya, Kamishna Jenerali wa Jeshi hilo, John Masunga, alisema pongezi hizo zitasaidia kuongeza ari na morali kwa askari wengine kutekeleza majukumu yao kwa ujasiri, weledi na kujituma zaidi.

Masunga, alisema pongezi hizo zitasaidia kuongeza ari ya utendaji kazi za jeshi hilo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Desemba mwaka jana Waziri Simbachawene alimwagiza Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Masunga kumpeleka askari huyo mwenye namba ZETM 3847 ofisini kwake kwaajili ya kumpongeza na kumshika mkono kwa kitendo cha ushujaa, ujasiri na upendo wake ambao amekuwa akiuonyesha wakati wa utekelazaji wa majukumu ya kuokoa maisha ya watu pamoja na mali zao.




Mkazi wa Dodoma Mjini akitafuta wanunuzi wa nyasi kwa ajili ya malisho ya mifugo barabara kuu ya Nyerere jana, aliuza Sh. 2,500 kwa toroli moja. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Madiwani waonywa kutegemea posho vikaoni

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, wametakiwa kuacha tabia ya kutegemea posho za vikao, badala yake wajikite kwenye shughuli za uzalishaji ikiwamo ya ujasiriamali, ufugaji na kilimo cha bustani za mboga.

Ushauri huo ulitolewa jana na Diwani wa Viti Maalumu (CCM), Jimbo la Mvumi Misheni Kata ya Iloje, Hilda Kadunda, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema madiwani lazima waonyeshe mfano mzuri kwa wananchi waliowachagua kwa kuonyesha kwa vitendo kazi mbalimbali za kuwaingizia vipato kama vile ujasiriamali, kilimo cha bustani na ufugaji.

Pia, alisema madiwani wakionyesha kwa vitendo shughuli hizo za uzalishaji za kujiingizia vipato, watawaokoa vijana ambao wamekata tamaa ya maisha ambao walikuwa wakitegemea kupata ajira toka serikalini.

"Madiwani wakijikita kwenye shughuli za kujiingizia kipato ni rahisi pia kushawishi vijana na watu wengine kuanzisha miradi itakayoweza kuwanyanyua kiuchumi na hatimaye kuondokana na umaskini," alisema.

Aliwataka kinamama, watu wenye ulemavu pamoja na vijana kuunda vikundi ambavyo vitawawezesha kuomba mikopo ambayo inatolewa na halmashauri za wilaya kwa ajili ya makundi mbalimbali.

"Fedha zipo kwenye halmashauri zetu, kinachotakiwa ni kuuunda vikundi mbalimbali vya kinamama, watu wenye ulemavu na vijana, ambavyo pia wahakikishe wamepata usajiri ili waweze kupata mikopo hiyo," alisema.

Aliwataka wakulima wa kata hiyo kuhakikisha wanapanda miti kwenye vyanzo vya maji na milimani ambako mazingira yameharibiwa kwa kukata miti ovyo.

Vile vile, aliwasisitiza wazazi na walezi watoto wote wenye haki ya kupata elimu wasiachwe nyumbani kwa vizingizio vya kukosa mahitaji, kwa kuwa wakiwafanyia hivyo watakuwa wamewanyima haki zao za msingi watoto.

Alisema serikali imewapunguzia wazazi na walezi mzigo mkubwa wa kusomesha watoto kwenye shule za serikali, na kwamba wanatakiwa kujipanga kuhakikisha watoto hao wanapata haki yao ya msingi ya elimu.





# TMDA yaendesha msako dawa za nguvu za kiume

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeanza kufanya misako maeneo yote ya mipakani ili kudhibiti uingizwaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopigwa marufuku zikiwamo dawa za kuongeza nguvu za kiume.

Mkurugenzi wa TMDA, Mitango Fimbo, ametoa kauli hiyo jana akiwa mkoani Mbeya kwa lengo la kukagua dawa zilizokamatwa na mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Alisema kuna wimbi la wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ambao wanafanya biashara ya kuuza kinyemela dawa zilizopigwa marufuku kuingizwa nchini, alisema mtandao huo ni mkubwa maeneo mbalimbali na kwamba wamejipanga kudhibiti.

**Kuna mtandao mkubwa wa baadhi ya wafanyabiashara wakubwa kujihusisha na uuzaji na usambazaji wa dawa zilizopigwa marufuku nchini.**

"TMDA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, tumefanikiwa kumkamata mfanyabiashara anayeuza dawa zilizopigwa marufuku zikiwa na madhara kwa binadamu, tumejipanga kudhibiti mtandao huo wa uingizwaji wa dawa na vifaa tiba kiholela, gari alilobebea dawa hizo bado liko mikononi mwa polisi," alisema Fimbo.

Fimbo alisema wale wote watakaobainika kujishughulisha na biashara hiyo ya magendo, watafikishwa kwenye vyombo vya sheria ikiwa ni pamoja na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi na kutumikia kifungo cha miaka mitano jela.

Aliongeza kuwa TMDA inaendelea na upelelezi wa kubaini mtandao wa wauzaji na wasambazaji wa dawa ambazo licha ya kuisha muda wake, lakini wanaongeza muda wa matumizi na kuhatarisha afya za watumiaji.

Alisema wanazo mbinu mbalimbali za kubadilisha mwonekano wa dawa hizo na kusambaza kwa wateja wao ambao bila kujua huzitumia.

Alionya tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kujihusisha na uuzaji wa dawa ambazo ziko kwenye mzunguko wa dawa zinazotolewa na serikali kwa kuwa hazipaswi kuuzwa kwenye maduka ya watu binafsi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kuna mtandao mkubwa wa baadhi ya wafanyabiashara wakubwa kujihusisha na uuzaji na usambazaji wa dawa zilizopigwa marufuku nchini.

Alisema anaandaa majina ya wafanyabiashara hao na kuyataja hadharani ili kukomesha biashara hiyo ya uingizwaji na usambazaji wa dawa zilizopigwa marufuku ikiwamo za kuongeza nguvu za kiume.

Aliwaomba wakazi wa Mbeya kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola ili kukomesha biashara hiyo ambayo inahatarisha afya za watumiaji na kuikosesha serikali mapato.

## Miche 1,000 kupandwa Shule ya Magufuli

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MICHE 1,000 ya miti ya aina mbalimbali inatarajiwa kupandwa katika Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Magufuli baada ya Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuipatia shule hiyo.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Cosmas Ndakidemi, alisema jana kuwa waliamua kutoa miche hiyo kwa lengo la kukuza na kutunza uhifadhi wa mazingira shuleni huko. Alisema miche hiyo itapandwa kuzunguka eneo lote la shule ambalo kwa sasa halina miti ya aina yoyote, wakiamini kupandwa kwa miche hiyo kutasaidia kukabiliana na upepo mkali.

Akizungumza wakati wa upandaji wa miche hiyo jana shuleni huko kulikoshuhudiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, mhifadhi huyo alisema mbali na kugawa miche kwa shule hiyo, pia wameandaa utaratibu wa kugawa kwa wananchi wenye uhitaji.

Akizundua mpango huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila, aliuomba uongozi wa Shule ya Magufuli kuongeza kasi ya upandaji wa miche hiyo.

Alisisitiza kila mwalimu kupata mche wake na kuandika jina ili iwe rahisi kutambua ni yupi atatunza mti wake utakapokuwa.

Aliwakumbusha pia kuzungumza na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania TARI Kituo cha Uyole kuomba miche ya matunda kwa ajili ya watoto shuleni kupata matunda.

Alisema matunda hayo yatakuwa ni sehemu ya lishe kwa watoto wawapo shuleni na kukabiliana na tatizo la udumavu.



Mkurugenzi wa Masoko na Huduma kwa Wateja wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Yesaya Mwakifulefule (kulia), akipewa maelezo na Mkurugenzi wa China Garage, Yang Jie (katikati) kuhusu moja ya magari ambayo yanatengenezwa baada ya kupata ajali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mkurugenzi wa bima aona shida wamiliki wa magari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKURUGENZI wa Masoko na Huduma kwa Wateja wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), amewashauri wamiliki wa vyombo vya moto nchini, yakiwamo magari, kuvikatia vyombo vyao bima, ili iwasaidie kufidiwa wanapopata ajali za barabarani zinazosababisha uharibifu wa mali.

Yesaya Mwakifulefule, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na maofisa wa shirika hilo kutoka makao makuu na wa Mkoa wa Mbeya walipofanya ziara ya kuwatembelea wadau wao.

Katika ziara hiyo, watendaji hao wa NIC walitembelea karakana mbalimbali za kutengeneza magari ambazo zinafanya biashara na shirika hilo ikiwamo ya China Garage iliyoko katika Kata ya Uyole jijini Mbeya.

Alisema ajali nyingi zimekuwa zikitokea barabarani kutokana na sababu mbalimbali ambazo baadhi yake huwa ni vigumu kuepukika, hivyo mmiliki wa chombo hicho kama hana bima, mali zake hupotea na hawezi kufidiwa.

Alizitaja baadhi ya sababu ya ajali hizo kuwa ni pamoja na ubovu wa barabara, uzembe wa madereva na ubovu wa vyombo hivyo na kwamba njia pekee ya wananchi kurejeshewa mali zao ni kuvikatia vyombo vyao bima.

"Sasa hivi ofisi za Shirika la Bima la Taifa (NIC) zipo katika kila mkoa nchini, hivyo tunawashauri wamiliki wa vyombo vya moto kuzitembelea ofisi zetu, ili tuwakatie, tunatoa huduma bora na kwa haraka kuliko kampuni lolote," alisema Mwakifulefule.

Alisema shirika hilo limekuwa likiaminika na wananchi na kwamba kwa mwaka limekuwa linawahudumia zaidi ya wateja 200 ambao ni wadau wao.

Mkurugenzi huyo alisema shirika hilo linatoa malipo ya bima kwa mtu anayepata ajali ndani ya siku saba kuanzia siku ajali inapotokea na hivyo akawashauri wananchi kuchangamkia fursa hiyo muhimu.

Baadhi ya wadau wa shirika hilo walilishukuru shirika hilo kwa kuwajali wateja wakidai kuwa linawasaidia kufanya ukarabati wa vyombo vyao pale vinapokuwa vimepata matatizo kwenye ajali.

Mkurugenzi wa China Garage, Yang Jie, alisema wamekuwa wanashirikiana na NIC kwa muda mrefu na kwamba wateja wengi wamekuwa wakipata haki zao kwa wakati.

Alisema wao huwa wanapelekewa maelezo ya vitu vyote vinavyohitajika kwa ajili ya ukarabati wa gari husika na hivyo kufanya matengenezo kwa kuzingatia ubora.

Alisema baadhi ya magari huwa yanatengenezwa kwenye gereji za mitaani ambako mafundi huwa wanaweka vifaa feki ambavyo huwa miongoni mwa sababu ya kutokea kwa ajali za barabarani.

Vilevile, alisema baadhi ya ajali hutokea kwa sababu wanaoendesha vyombo hivyo wanakuwa wamelewa kiasi kwamba wanapoteza umakini kwenye uendeshaji.

Baadhi ya wanufaika wa bima, waliwasihi wamiliki wa vyombo vya moto kujiwekea utaratibu wa kukata bima ili wafidiwe wanapopata matatizo.



# Mwinyi awapa majukumu MaDC

**Na Hawa Aabdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wakuu wa wilaya aliowaapisha kufanya kazi kwa kujituma kwa kutatua matatizo yanayowakabili wananchi katika maeneo yao.

Dk. Mwinyi alitoa kauli hiyo katika hafla ya kuwaapisha wakuu wa wilaya wapya na wa zamani aliowateuwa hivi karibuni, hafla ilifanyika hapo juzi Ikulu Mjini Unguja.

Aliwaasa kutokaa ofisini na badala yake kushuka zaidi kwa wananchi kusikiliza matatizo yanayowakabili na changamoto mbalimbali ili zitatuliwe kwa haraka.

Rais Mwinyi alisisitiza kuwa kuna matatizo maalum ambayo yanataka kuwekewa mkazo yakiwamo ya migogoro ya ardhi kwa kuwa kila siku wanapokea taarifa ya kuwapo kwa migogoro hiyo.

**Siku za nyuma kulikuwa na mashindano kati ya wilaya, mkoa na mkoa, shkuli na skuli ambalo lilikuwa likiwahamasisha wanafunzi hivyo wakati umefika kuinua elimu nchini na lazima kuanza katika ngazi za chini.**

"Hakikisheni mnaipitia na kutosikiliza migogoro yote na mnatoa haki bila kuonea upande wowote yapo mengine yatakuwa juu ya uwezo wenu kwa sababu yameamuliwa katika ngazi ya wizara au mkoa hakikisha lipo juu ya uwezo wako unalipeleka ngazi husika, tufike sehemu migogoro ya ardhi inayosabishwa na ngazi za chini kwa masheha mnaishughulikia na kuimaliza mara moja," alisisitiza.

Alisisitiza suala la usafi wa mji na masoko linalotokana na tatizo la manispaa, lakini kama mkuu wa wilaya ana kila sababu ya kuhakikisha wilaya zao zinakuwa safi wakati wote kwa kuwa Zanzibar inatembelewa na watalii.

Pia, aliwaagiza wakuu wa wilaya hao kulivalia njuga suala la udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto kwa kushirikiana pamoja kwa kuanza katika jamii pamoja na vyombo vyote vinavyohusika ili kuja na mpango mpya wa kushughulikia jambo hilo na kutafuta njia muafaka ya kuondoa vitendo hivyo nchini.

"Sasa tunataka kuwa na mpango mpya wa kuondoa jambo hili kwani kila kukicha unasikia matukio ya udhalilishaji yanazidi na hatuwezi kuliachia kama hivi lilivyo ni lazima kutafuta njia muafaka suala la udhalilishaji kwa watoto na wanawake," alisisitiza.

Rais Mwinyi aliwataka wakuu hao ni kuinua viwango vya elimu ndani ya wilaya zao ikiwamo kuhakikisha miundombinu, idadi ya walimu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia vyote vinapatikana ili watoto waweze kupata elimu bora na itakayopelekea ufaulu mzuri katika mitihani yao Zanzibar.

"Siku za nyuma kulikuwa na mashindano kati ya wilaya, mkoa na mkoa, shkuli na skuli ambalo lilikuwa likiwahamasisha wanafunzi hivyo wakati umefika kuinua elimu nchini na lazima kuanza katika ngazi za chini," alisema.

Aliwataka wakuu hao kuwa wabunifu kwa kuondoa kero za wananchi na kutengeneza utaratibu mzuri wa kusikiliza kero na kutoa ufumbuzi.

Akizungumzia suala la ulinzi na usalama Rais Mwinyi alisema kama wenyeviti wa kamati za ulinzi na usalama katika ngazi ya wilaya, wana kila sababu ya kuhakikisha kuna ulinzi na usalama wa kutosha kwa kuwa bila ya usalama hakuna maendeleo yatakayopatikana.

Kwa upande wao viongozi hao waliahidi kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kuhakikisha wanayafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa ili kuona wananchi wanapata maendeleo.

Walioapishwa ni pamoja na Mkuu wa Wilaya Mjini, Rashid Simai Msafaka, Mkuu wa Wilaya Magharibi 'B', Hamida Mussa Khamis, Kaskazini 'A', Sadifa Juma Khamis, Kaskazini 'B' Aboud Hassan Mwinyi, Wilaya ya Kusini Rashid Makame Shamsi, Wilaya ya Kati Marina Joel Thomas.

Wengine ni Mgeni Khatib Yahya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Wete, Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, CDR Mohammed Mussa Seif, Mkuu wa Wilaya ya Chakechake Abdallah Rashid Ali na Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Issa Juma Ali.

## Ataka udhibiti bidhaa zenye madhara kwa binadamu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, amewataka watendaji wa wakala wa chakula, dawa na vipodozi Zanzibar, kudhibiti uingiaji wa bidhaa zisizofaa nchini ili kulinda afya za binadamu.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha sekta ya afya kwa maslahi ya nchi ambao wanapaswa kuzilinda kwa kuzuia uingiaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi wa jengo la maabara ya wakala wa chakula, dawa na vipodozi, Mombasa ikiwa ni shamrashamra ya kuadhimisha miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ni vyema wakawa makini kudhubiti uingizaji na uuzwaji wa bidhaa ambazo zimemaliza muda wake katika maduka mbalimbali hususani bidhaa zza vyakula kama vile mchele, ngano pamoja na bidhaa nyingine za vyakula ambavyo vipo katika vifungashio maalum.

Alisema, ni vyema wakazingatia utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na kutoa huduma bora na kuchangia maendeleo ya nchi pamoja na kuimarisha ukuaji wa wajasiriamali.

Aliwashukuru washirika kwa kukubali kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza mradi huo ambao ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Akitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maabara ya ZFDA, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Halima Maulid Salum, alisema jengo hilo linatekelezwa kwa awamu mbili ambapo litakuwa ni jengo la ghorofa tatu.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akiwapongeza wasimamizi wa mradi mkubwa wa ujenzi wa jengo la Shule ya Sekondari ya Donge kwa kutumia gharama ndogo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Elimu bila malipo fursa kuboresha kiwango'

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Suleiman Abdulla, amesema tangazo la elimu bila ya malipo lililotolewa baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 lilikuwa na maana ya kuongeza fursa za kupata elimu iliyo bora kwa wote.

Alisema hayo jana wakati wa akifungua Shule ya Sekondari ya Donge, Mkoa Kaskazini Unguja ikiwa ni shamra shamra za maadhimisho ya kusherehekea miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964.

Alisema elimu bora na ya kiwango ndiyo inayomwezesha mwanadamu hasa watoto wa taifa la Tanzania kukabiliana vyema na matatizo mbalimbali wanayokumbana nayo katika maisha yao, wazazi na taifa kwa ujumla.

Hemed alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya usimamizi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, itaendelea kutoa elimu bila ya malipo kwa taaluma ya msingi hadi sekondari ili kuwawezesha wanafunzi wenye sifa kupata elimu bila ya vikwazo.

Aliwapongeza wananchi wa Donge kwa jitihada, mshikamano, ushirikiano na ustahimilivu wao wa kuunga mkono jitihada za serikali katika kujiletea maendeleo hasa katika sekta muhimu ya elimu na sasa jamii inashuhudia matunda hayo.

Alisema Donge imekuwa mfano mzuri wa kuigwa na jamii nyingine nchini kwa kujenga shule kubwa na ya kisasa ya ghorofa jambo ambalo limesaidia kupunguza tatizo la ufinyu wa nafasi katika elimu ndani ya Wilaya ya Kaskazini B.

Alisema ujenzi wa shule hiyo ni kielelezo cha juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi wake ikiwa ni mkakati wa kuhakikisha nafasi za masomo kwa watoto wa visiwa vya Unguja na Pemba zinapatikana katika maeneo yote.

"Fursa sawa za kupata elimu ni miongoni mwa malengo ya Mapinduzi yetu ya mwaka 1964 ambapo hivi sasa tumo katika kuadhimisha miaka 57," alisema.

Alisema hivi sasa Wilaya ya Kaskazini B ina jumla ya shule 11 za sekondari ikiwa ni maendeleo makubwa na matunda ya Mapinduzi ya Mwaka 1964 na wananchi wanapaswa kujivunia kwa vile elimu imekuwa ikiwafikia wananchi walipo.

Alisisitiza umuhimu wa wazazi, walezi, walimu na kamati za maskuli nchini kuendelea kushirikiana hatua itakayorahisisha upatikanaji wa maendeleo ya haraka ya watoto wao.

Aliwakumbusha wanafunzi wakayatumia mazingira bora wanayowekewa na serikali kwa kuzidisha juhudi za masomo zitakazozalisha matokeo mapya ya viwango vya juu katika mitihani yao ya taifa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAMISAA MARIA MLINGI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 300 BFB MITSUBISHI/ROSA.** Chassis namba BE **433F40902.** Engine namba **B 451120.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **TAARIFA YA POLISI: D A R / M A G / R - B/893493/2020**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SAUDA RASHIDI HAMISI** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index namba **P0203-0301** kilichotolewa na **IRINGA GIRLS CENTRE** mwaka **2011**. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0203-0265** kilichotolewa na **IRINGA GIRLS CENTRE** mwaka **2012.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Control No: 9910820039577.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ZAITUNI KAZERI BAKARI** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba S.0328/0664 iliyotolewa na **MAWENZI SEKONDARI** mwaka 2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: DAR/CHU/R-B/857534/2020.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**FRANK DONALD MUSHI** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 087979** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **07/02/2019.** Muda wake wa kuisha matumizi ni tarehe **06/02/2029.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: OB 1762/08/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI




**DOREEN PETER ASSENGA** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha kidato cha nne chenye index namba S0205-0038 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIBOSHO GIRLS SEKONDARI** mwaka **2014.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: WMB/RB/21/2021.**

## KUFUNGA KAMPUNI

Tunapenda kutangazia umma wote kuwa kampuni ya **PIVOTAL LIMITED** yenye namba ya usajili **13770195 imefungwa baada ya kikao cha wakuregenzi cha mnamo tarehe 20/12/2020.** Kwa yeyote atakaye kuwa anaidai kampuni awasiliane nasi kwenye simu namba 0746820396.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI-MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi **No; 01/2021**
Ombi la **MARTHA TUMAINI** MSHASHI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **HAPPY MSHASHI BWIRE.** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **08/01/2021** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **04/01/2021**



Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marufuku safari za kuingia na kutoka mjini Kigali

**Kigali, RWANDA**

NCHI ya Rwanda imepiga marufuku usafiri wa umma na binafsi wa kuingia na kutoka mji mkuu, Kigali.

Serikali ya nchi hiyo, imetangaza kuwa hali hiyo inatokana na hali ya kutisha ya maambukizi ya virusi vya corona.

Katika wiki moja, Rwanda ilirekodi watu 30 kufariki dunia, kutokana na ugonjwa huo.

Kulingana na kikao cha baraza la mawaziri, hatua ya kupiga marufuku usafiri wa umma na binafsi kati ya wilaya na mji mkuu Kigali, imeanza kutekelezwa jana, kwamba inadhibiti wimbi jipya la maambukizi ya virusi vya corona nchini Rwanda.

Serikali ilisema hiyo ni kutokana na kuongezeka kwa visa vya maambukizi pamoja na vifo vya watu.

Takwimu zinazotolewa na maofisa wa afya wa Rwanda, zinaonyesha kwamba jumla ya watu 105, wameshafariki dunia kutokana na Covid-19 huku nusu yao wakipoteza maisha Desemba mwaka jana.

Akizungumza na radio ya taifa, Dk. Tharcisse Mpunga anayesimamia huduma ya msingi ya afya, alieleza kwamba katika kiwango hicho, nchi inapaswa kutekeleza sheria ya kutototoka nyumbani kote nchini.

"Hatukupenda maisha yasimame kabisa."

Dk. Mpunga aliongeza kwamba, hali ilivyo sasa wagonjwa mahututi wanakufa haraka wakiwamo vijana.

Kadhalika, serikali ya Rwanda, ilitangazwa kuwa watalii wa ndani na wa kimataifa, wanaweza kusafiri kote nchini baada ya kupima Covid-19 na kuthibitisha kuwa hawana maambukizi ya ugonjwa huo.

Maofisa wa Afya wa Rwanda, wanaamini kuwa ongezeko la maambukizi huenda lilichangiwa na sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya na watu walisafiri kwenda maeneo yao asilia.

***BBC***



Mtoto akisoma nukta nundu shuleni nchini Uganda. Umoja wa Mataifa (UN), unasema watu wenye ulemavu wa kuona na uoni hafifu, wanakabiliwa na viwango vya juu vya umaskini, kutengwa na ukatili. **PICHA/UNICEF**

# UN: Wenye ulemavu wa kuona wana viwango vya juu umaskini, ukatili

**Washington, MAREKANI**

WAKATI Umoja wa Mataifa (UN), ukiadhimisha Siku ya Nukta Nundu Duniani kila Januari 4, shirika hilo, limesema, watu wenye ulemavu wa kuona wako hatarini kukabiliwa na viwango vya juu vya umaskini ikiwamo kutengwa na kufanyiwa ukatili.

UN, limesisitiza umuhimu wa nukta nundu ili kufikisha habari kwa mfumo huo, kwa watu wenye ulemavu wa kutoona na watu wenye uoni hafifu, wahabarike.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO), takriban watu bilioni 2.2 duniani kote wana ulemavu wa kutoona, kati yao hao bilioni moja, wana ulemavu wa kuona ambao ungezuilika au kutibiwa.

Siku ya Nukta Nundu Duniani huadhimishwa kila Januari 4 baada ya kupitishwa kwa azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Desemba, mwaka 2018.

Tarehe hiyo, inalingana na kuzaliwa kwa Louis Braille, ambaye wakati akiwa na umri wa miaka 15, alizindua mfumo wa kusoma na kuandika wa nukta nundu, kwa ajili ya matumizi na watu hao.

Nukta nundu husomwa kwa kupitisha ncha ya vidole juu ya nukta kati ya moja hadi sita zilizochorwa, ambazo zinawakilisha herufi, nambari pamoja na alama za muziki na hisabati.

Mkataba wa UN, kuhusu haki za watu wenye ulemavu, CRPD, unataja mfumo wa nukta nundu, kama njia ya mawasiliano muhimu katika elimu, uhuru wa kujieleza, kupata taarifa na ujumuishwaji katika jamii.

Mfumo wa nukta nundu umerekebishwa katika kipindi cha miaka ya 1949, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), lilifanya utafiti ukilenga kuoanisha mfumo wa nukta nundu, na kwamba corona imeongeza tatizo kwa kundi hilo na kuwatenganisha na jamii.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), lilitoa mwongozo kwa lugha mbalimbali na mifumo inayofikika, ikiwamo nukta nundu kuhusu mambo ya kuzingatia kwa watoto na watu wazima walio na ulemwavu katika kukabiliana na covid-19 ***UN***

# Total yaondoa wafanyakazi kuhofia mashambulio kigaidi

**Cabo Delgado, MSUMBIJI**

KAMPUNI ya mafuta ya Total imewaondoa maelfu ya wafanyakazi wake katika visima vya mafuta, vilivyopo Kaskazini mwa Msumbiji.

Hatua hiyo ni baada ya wanamgambo watiifu kwa kundi la Islamic State (IS), kutishia kushambulia mji muhimu katika eneo hilo.

Vyombo vya habari vinasema kwamba, wanamgambo hao walisambaza vikaratasi vinavyotishia kushambulia eneo la Palma katika mkoa wenye utajiri wa mafuta wa Cabo Delgado.

Tishio hilo lilisababisha Total kuwaondoa wafanyakazi wake katika eneo la Afunsi karibu na Palma, linaloongoza kwa ujenzi wa kiwanda cha gesi chenye thamani ya Dola bilioni 14.9.

Mtandao wa Carta de Mocambique, umesema kwamba wapiganaji hao walikabiliana na vikosi vya serikali karibu na Palma, Januari Mosi, mwaka huu.

Mkoa wa Cabo Delgado, ni nyumbani kwa Rais Fillipe Nyusi, ukipakana na Tanzania, umekumbwa na ghasia zinazotekelezwa na wapiganaji hao, tangu mwaka 2017.

***TRT***

# Mpaka Saudia, Qatar wafunguliwa

**Kuwait City, KUWAIT**

WAKATI viongozi wa nchi za Ghuba ya Uarabu, wakifanya mkutano wa kilele jana, Saudi Arabia imeifungulia mipaka ya anga na ardhini, Qatar, kupunguza uhasama wa zaidi ya miaka mitatu katika ukanda huo.

Taarifa kuhusu suala hilo, ilitangazwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Kuwait, juzi, ambayo ilieleza kuwa kuanzia wiki hii, anga, nchi kavu na bahari kati ya Saudi Arabia na Qatar, itakuwa wazi tangu mwaka 2017, ilipofungwa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Kuwait, Ahmed Nasser al-Mohammed al-Sabah, alisema Kiongozi wa Kuwait, Nawaf al-Ahmed al-Sabah, ndiye ametoa mapendekezo yaliyosaidia kufunguliwa tena kwa mipaka baina ya Saudi Arabia na Qatar.

Waziri huyo alisema ni baada ya mazungumzo ya mrithi wa ufalme wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman

Katika mazungumzo hayo, imehakikishwa na kusisitizwa kuwa kila upande unataka muungano na kwa kauli moja wanataka kusaini ilani ya al-Ula, ambayo itafungua ukurasa mpya wa uhusiano wa kidugu usio na vizingiti," alisema waziri huyo.

"Kulingana na mapendekezo ya kiongozi wa Kuwait, Nawaf Ahmad al-Sabah, imeamuliwa kuwa mipaka ya angani, ardhini na baharini kati ya Saudi Arabia na Qatar iwe wazi."

***DW***



# INTER WAWANIA KUMSAJILI ORIGI

**MILAN, Italia**

KLABU ya Inter Milan inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili, Divock Origi kutoka Liverpool.

Kwa mujibu wa Sky Sport Italia, kocha Antonio Conte anataka kumsajili msaidizi wa Romelu Lukaku, ambaye amekuwa katika kiwango bora kwa kufunga mabao 15 katika mechi 17 msimu huu.

Na Origi ndiye anayeonekana kuwa chaguo namba moja kwa Conte kwa ajili ya kumsaidia Lukaku kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu.

Inter ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ikipitwa pointi moja na vinara AC Milan ambao hadi sasa hawajapoteza mchezo wowote kwenye ligi.

Wolves na Newcastle pia wamehusishwa na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, ambaye anaonekana kutaka kuondoka pale kwenye viunga vya Anfield.

Inaaminika kuwa Majogoo nao wako tayari kuachana na shujaa wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Januari hii na wanasikiliza ofa kwa mshambuliaji huyo, wakati kocha, Jurgen Klopp akitafuta fedha za kusajili beki.

Origi ataungana tena na raia mwenzake Lukaku ikiwa atajiunga na Inter Milan, ambao wanaangalia uwezekano wa kumchukua kwa mkopo.

Origi, aliyejiunga na Liverpool kwa pauni milioni 10 mwaka 2014 akitokea Lille ana mkataba hadi 2024, na ni kipenzi thabiti cha mashabiki Anfield kwa misimu miwili iliyopita, lakini amecheza mara nane tu kwenye mashindano yote msimu huu.

## IBRAHIMOVIC AREJESHA MATUMAINI MILAN

**MILAN, Italia**

MASHABIKI wa AC Milan wanatumaini kuwa nyota wao Zlatan Ibrahimovic atakuwa fiti kurejea dimbani kwenye mchezo wa leo, Jumatano dhidi ya Juventus.

Nyota huyu mwenye umri wa miaka miaka 39, hajaweza kuingia dimbani tangu Novemba 22, mwaka jana, alipopata jeraha kwenye mechi ambayo Milan walishinda ugenini dhidi ya Napoli.

Milan wanakutana uso kwa uso na Juventus Jumatano, na kwa mujibu wa chapisho la nyota huyu kwenye mitandao, amerejesha matumaini ya mashabiki juu ya kurejea kwake kwenye mechi hiyo.

Nyota huyu amechapisha video fupi akiwa mazoezini na kuandika maneno yanayoashiria muda si mrefu huenda akawa fiti dimbani.

Katika video yake aliyochapisha aliambatanisha maneno ya "Tick tock tick tock."

Nyota huyu wa zamani wa Inter Milan na Manchester United, juzi alifanya mazoezi ya peke yake.

Hata hivyo, baada ya ushindi wa Jumapili kocha Stefano Pioli aliweka wazi kuwa hana uhakika kama nyota huyo atarejea haraka na hawakuwa na mpango wa kumharakisha.

## SOUTHAMPTON YAWEKA REKODI EPL



**LONDON, England**

KLABU ya Southampton imeweka rekodi ya aina yake kwenye Ligi Kuu England baada ya usiku wa kuamkia jana kuifunga Liverpool bao 1-0.


Baada ya ushindi huo, Southampton imeweka rekodi ya kwanza kwa kuwafunga mabingwa wote saba kwenye misimu inayofuata baada ya kubeba taji la Ligi Kuu ya England, EPL.

Manchester United, Manchester City, Arsenal, Chelsea, Leicester City, Blackburn Rovers na sasa Liverpool wameambulia vipigo kutoka kwa Southampton kwenye misimu iliyofuata baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu.

Liverpool walijikuta wakiangukia pua kunako dakika ya pili ya mchezo huo, wakati Danny Ings alipoitumia vema nafasi aliyoipata na kumuadhibu golikipa, Alisson Becker.

Hicho ni kipigo cha pili kwa Liverpool msimu huu na kimewafungulia mwaka 2021 vibaya, mchezo unaofuata watawakaribisha Man United katika dimba la Anfield.

Hata hivyo, Liverpool inaendelea kuongoza msimamo wa ligi hiyo pamoja na Manchester United kwa tofauti ya mabao.




# GUARDIOLA
## ABADILI UAMUZI KUSTAAFU

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema anafikiria kukaa kwa muda mrefu katika kazi yake ya ukocha kinyume cha alivyokuwa anafikiria mwanzoni.

Guardiola mwenye umri wa miaka 49, mara kadhaa amekuwa akilalamika juu ya soka kumnyima muda wa kufanya mambo yake mengine nje ya soka.

Lakini sasa ameibuka na kusema kwamba, anaweza kukaa kwa muda mrefu zaidi kwenye kazi yake hiyo tofauti na alivyokuwa anafikiria mwanzo.

"Mwanzoni nilikuwa nasema nitastaafu karibuni, lakini sasa nafikiria nitastaafu nikiwa mkubwa," alisema Guardiola akinukuliwa na Daily Mail.

"Sijui nini kitatokea, lakini naona kabisa kwamba, siwezi kustaafu hivi karibuni kama nilivyokuwa ninawaza mwanzo," alisema Guardiola.

Kocha huyo raia wa Hispania aliingia mkataba mpya wa miaka miwili na matajiri hao wa Jiji la Manchester Novemba mwaka jana, ambapo ameshinda mataji sita makubwa klabuni hapo.

## KLOPP: HAKUNA WA KULAUMIWA LIVERPOOL KWA KICHAPO

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema hakuna wa kumlaumu kwa kupoteza mchezo wao wa Ligi Kuu England mbele ya Southampton.




Liverpool ilichezea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Southampton juzi Jumatatu usiku kwenye Ligi Kuu England.

Wakiwa pale kwenye Uwanja wa St Mary's walikubali kuyeyusha pointi tatu baada ya kufungwa bao la mapema dakika ya pili kupitia kwa Danny Ings.

Kichapo hicho kinawafanya mabingwa hao watetezi kuwa sawa kwa pointi na Manchester United ambao nao wana pointi 33, lakini United ina mchezo mmoja mkononi.

Wao Southampton wapo nafasi ya sita na pointi zao ni 29 baada ya kucheza jumla ya mechi 17.

"Sidhani kama kuna mtu wa kumlaumu kwa matokeo haya," alisema Klopp baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulianza vibaya, na tukaadhibiwa kwa kosa moja, lakini siwezi kusema ni mchezaji gani wa kulaumiwa, tumepoteza nafasi muhimu kwenye mchezo muhimu," alisema Klopp.

"Tulipata nafasi nyingi, lakini hatukuweza kuzitumia, hivyo tatizo ni la kwetu na wachezaji walionekana kujaribu kupambana, lakini hawakufanikiwa."

Kwenye mchezo huo, Liverpool ilipiga jumla ya mashuti 17 huku Southampton wakipiga jumla ya mashuti saba tu katika hayo ni shuti moja la Liverpool lililenga lango huku Southampton mashuti matatu yakilenga lango.



## LUKAKU AFIKIA REKODI YA RONALDO DE LIMA

**MILAN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Romelu Lukaku, ameifikia rekodi iliyowekwa na Ronaldo de Lima klabuni hapo.

Ronaldo alifunga mabao 50 katika mechi 78 kwa klabu hiyo na hakuna mchezaji mwingine aliyeifikia rekodi hiyo.

Lukaku alifanikiwa kuifikia rekodi ya gwiji huyo ya kufunga mabao 50 katika mechi 70 alizoichezea Inter Milan.

Ronaldo aliweka rekodi hiyo wakati akiwa na umri wa miaka 23, lakini Lukaku ameifikia akiwa na umri wa miaka 27.

Katika mchezo dhidi ya Crotone, Jumamosi ambao walishinda mabao 6-2, mshambuliaji huyo alifanikiwa kufunga bao dakika ya 64 na kufikisha mabao 50 tangu ajiunge na Inter.

Rekodi hiyo ilikuwa inashikiliwa na Ronaldo ambaye alikuwa mchezaji wa kwanza ambaye si raia wa Italia kufunga mabao 50 katika mechi 78 za kwanza.

Lukaku amekwishacheza jumla ya mechi 70 tangu ajiunge na klabu hiyo akitokea Manchester United.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RAMOS SASA HURU KUONDOKA MADRID

**Klabu za Ligi Kuu England, Man City, Man United na Liverpool ni miongoni mwa zinazotajwa...**

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos kwa sasa yupo huru kuzungumza na klabu za Ligi Kuu ya England ama kwingineko nje ya nchi baada ya Real Madrid kuonyesha kusuasua kumpa mkataba mpya, kwa mujibu wa ESPN.

Real Madrid ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wanaweza kumpoteza nahodha wao huyo, kwani mkataba wake unamalizika mwisho mwa msimu huu.

Na kwa mujibu wa sheria za usajili, Ramos kwa sasa amebakiza miezi sita katika mkataba wake na anaweza kuzungumza na klabu yoyote kuhusu uhamisho wake.

Klabu za Ligi Kuu England, Manchester City, Manchester United na Liverpool ni miongoni mwa zinazotajwa kuhusishwa na nyota huyo wa timu ya Taifa ya Hispania.

Awali Kocha Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane, alibainisha kwamba, anataka Ramos abaki katika klabu hiyo, huku akiungwa mkono na rais wake.

Lakini hadi sasa kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania, hakuna mazungumzo yoyote yaliyofanyika kati ya mchezaji huyo na Real Madrid.

Ramos ameisaidia Real Madrid kushinda mataji matano ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, tangu ahamie pale Santiago Bernabeu akitokea Sevilla mwaka 2005.

Beki huyo wa kati amecheza mechi 666 kwa 'Blancos' hao, akifunga mabao 100, na licha ya ukweli kwamba atafikisha umri wa miaka 35 Machi mwaka huu, bado ni moja ya majina ya kwanza kwenye karatasi ya kocha Zidane.

Kwa kuwa dirisha la msimu wa baridi sasa limefunguliwa, Ramos anaweza kujadili makubaliano ya kabla ya mkataba na timu yoyote itakayochagua kufanya hivyo, na Madrid wakiwa katika hatari kubwa ya kupoteza jembe hilo kama hawatampa dili mpya.

Luka Modric na Lucas Vazquez pia watakuwa wachezaji huru ikifika Juni kama ilivyo kwa Ramos, lakini Zidane alionyesha hamu ya kuona wachezaji hao wakibaki katika mji mkuu wa Hispania na Ramos kwa siku zijazo.

## KWA UFUPI

**DE BRUYNE KUGOMEA MKATABA**

KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 29, anatarajiwa kukataa ofa ya kuongeza mkataba pale Manchester City na ana wasiwasi kuhusu kasi ya klabu hiyo katika mazungumzo ya kumpatia mkataba mpya wa miaka mitano. ***(Times)***

**SPURS KUTOMUACHIA DELLE**

KLABU ya Tottenham Hotspur haiko tayari kumuuza ama kumtoa kwa mkopo kiungo wa kati wa England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, mwezi huu. Lakini golikipa wa Argentina, Paulo Gazzaniga mwenye miaka 29 na beki wa England, Danny Rose mwenye miaka 30 wataruhusiwa kuondoka. ***(Sky Sports)***

**MAN CITY WAMTAKA RAMOS**

MANCHESTER City wanachunguza hali ya beki Sergio Ramos katika klabu ya Real Madrid, wakiwa na lengo la kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 kutoka Hispania atakayekuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(ESPN)***

**LAMPARD KUVUMILIWA CHELSEA**

CHELSEA ipo tayari kumpatia muda zaidi kocha Frank Lampard, lakini hali hiyo inaendelea kuchunguzwa huku Thomas Tuchel, Max Allegri, Brendan Rodgers na Ralph Hasenhuttl wakifikiriwa kama mbadala iwapo atafutwa kazi. ***(Independent)***

**SHEVCHENKO KUMRITHI LAMPARD**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Chelsea, Andriy Shevchenko, ambaye kwa sasa ndiye kocha wa timu ya Taifa ya Ukraine, pia anafikiriwa kujaza pengo la Frank Lampard iwapo atafukuzwa. ***(Le10 Sport)***

**ARSENAL KUTOMUUZA ELNENY**

ARSENAL haina mpango wa kumuuza Mohamed Elneny mwenye umri wa miaka 28, katika dirisha dogo la mwezi huu, huku klabu kadhaa zikionyesha nia ya kumtaka. ***(Football London)***

**JUVENTUS HAIMTAKI OZIL**

ARSENAL wamewapa ofa Juventus ya kiungo wao wa kati, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, lakini mabingwa hao wa Italia wanamuona mchezaji wa Sweden, Dejan Kulusevski mwenye miaka 20 kama mchezaji bora zaidi kwao. ***(CBS Sports)***

**BARCA YAWINDA NYOTA**

BARCELONA inawalenga kiungo wa kati wa Liverpool na Uhalonzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, beki wa kati wa Manchester City na Hispania, Eric Garcia mwenye miaka 19, na mshambuliaji wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay, 26.

**ROJO, BOCA JUNIORS WATETA**

MLINZI wa Manchester United na Argentina, Marcos Rojo, mwenye umri wa miaka 30, amefanya mazungumzo na klabu ya Boca Juniors ya nyumbani kwao, ingawa bado hawajaafikiana makubaliano. ***(Mail)***

**ARSENAL WAMTAKA BUENDIA**

ARSENAL inachunguza hali ya kiungo wa kati wa Argentina, Emi Buendia, lakini bado hawajawasilisha ombi rasmi la mchezaji huyo wa Norwich mwenye umri wa miaka 24. ***(Football London)***

**BAILLY AISHAWISHI UNITED**

KIWANGO cha mlinzi wa Ivory Coast, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 26, kinaweza kuishawishi Manchester United kutotafuta beki mwingine wa kati mwezi huu. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

# ZAHERA ASHIKILIA MPINI KOCHA MKUU GWAMBINA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kumfungashia virago Novatus Fulgence, uongozi wa Klabu ya Gwambina, umesema wanamsubiri Mkurugenzi wa Ufundi, Mwinyi Zahera ili kuendesha mchakato mpya wa kupata kocha mkuu wa kukinoa kikosi hicho.

Gwambina imemtimua Fulgence aliyeipandisha timu hiyo Ligi Kuu na kuiwezesha kupambana kwenye mechi 17 msimu huu ikishinda michezo minne, sare saba na kupoteza michezo sita wakati huu ikiwa nafasi ya 14 na pointi zake 19 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Gwambina FC, Daniel Kirahi, alisema bodi ilikutana jana (juzi), kujadili tathimini ya duru la kwanza na kutokana na mwenendo mbovu wa timu hiyo, wameamua kuachana na Fulgence.

Alisema kwa sasa timu hiyo itakuwa chini ya walimu wawili, Seleman Kisendi na Hassan Salum, ambao walikuwa sehemu ya benchi la ufundi na wataendelea na majukumu ya kukiongoza kikosi hicho.

"Hao wawili wataendelea kubaki na timu hadi hapo Zahera atakaporejea nchini kwa ajili ya mchakato wa kupata kocha mkuu atakayerithi nafasi ya Fulgence.

"Zahera hayupo nchini, alienda kwao kwa ajili ya matatizo ya kifamilia, anatarajia kurudi kati ya Januari 6 au 7, mwaka huu," alisema Kirahi.

Kuhusu malalamiko yaliyotolewa na Zahera kupitia chombo kimoja cha habari jijini Dar es Salaam (si Nipashe) juu ya kutoshirikishwa katika usajili wa wachezaji kwenye dirisha hili dogo, Mrisho Ngassa, Salim Aiyee na Mohammed Mussa kutoka Malindi ya Zanzibar, Kirahi alisema si kweli.

"Hakuna jambo ambalo tunalifanya bila kumshirikisha Zahera, kama tungekuwa hatufanyi hivyo nina imani taarifa angeziwasilisha kwa mkurugezi wa bodi au hata kwangu," alisema Karahi.

IKO HIVI...



Kocha wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije (kushoto), akitoa maelekezo kwa wachezaji wake wakati wa mazoezini katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam juzi, timu hiyo inajiandaa na mechi mbili za kirafiki dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zitakazopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Januari 10 na 13, ikiwa ni maandalizi ya fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zitakazofanyika nchini Cameroon kuanzia Januari 16 hadi Februari 7, mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hitimana ataka Mapinduzi Cup Mtibwa Sugar

**Na Saada Akida**

WAKATI jana ikifungua pazia la mashindano ya 15 ya Kombe la Mapinduzi, mabingwa watetezi Mtibwa Sugar, wamesema kuvurunda kwao kwenye Ligi Kuu Bara, kamwe hakuwezi kuwa sababu ya kushindwa kutetea ubingwa wao wa michuano hiyo iliyoanza kutimua vumbi visiwani Zanzibar.

Mtibwa Sugar ambayo imekuwa ikianza vizuri Ligi Kuu Bara, msimu huu imeshindwa kuonyesha makali yake kwenye mzunguko wa kwanza, baada ya kumaliza na pointi 22 zilizotokana na kushuka dimbani mara 18 ikishinda sita, sare nne na kupoteza mechi nane, hivyo kushika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Mwaka jana Mtibwa Sugar ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Zuber Katwila, ilitwaa ubingwa huo kwa kuifunga Simba kwenye mechi ya fainali, lakini mwaka huu Kocha Mnyarwanda Thierry Hitimana, aliyerithi mikoba ya mzawa huyo, ndiye mwenye jukumu la kuhakikisha inatetea ubingwa huo.

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kufungua michuano hiyo dhidi ya Chipukizi ya Zanzibar kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Amaan, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Hitimana, alisema watawakosa wachezaji wanne, lakini hilo haliwezi kuwaathiri katika malengo yao ya kutetea ubingwa huo.

Alisema mwendelezo wa kutofanya vizuri katika michezo yao ya ligi imekuwa changamoto kwao, hivyo mbali na kutaka kutetea ubingwa wa michuano ya Kombe la Mapinduzi, pia wataitumia kufanyia kazi makosa yao kabla ya kurejea Tanzania Bara kuendelea na Ligi Kuu.

"Tutaitumia kufanyia kazi upungufu wetu, lakini nawajenga kisaikolojia wachezaji wangu kuhakikisha wanapambana kutumia vizuri michuano hiyo kutetea ubingwa wetu," alisema Hitimana.

Alisema mbali na wachezaji wawili waliotwa Stars, pia atawakosa wengine wawili, Hassan Kessy na Salum Kihimbwa ambao ni majeruhi.

Hitimana alisema ni wachezaji muhimu ila hawatakuwa katika mipango yake kwenye michuano hiyo kwa sababu wanatakiwa kukaa nje kwa muda wa siku 11.

# Mchezaji Yanga amfuata Mkwasa

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI kinda wa Yanga, Adam Kiondo, amejiunga na kocha wa zamani wa timu hiyo, Boniface Mkwasa, katika klabu ya Ruvu Shooting kwa mkopo wa miezi sita, lengo likiwa ni kwenda kulinda kipaji chake.

Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, amesema mchezaji huyo ambaye kwa sasa yupo na kikosi cha Yanga kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, baada ya mashindano hayo kumalizika atajiunga na Ruvu Shooting kwa mkopo.

"Ni kweli mchezaji wetu wa kikosi cha pili, Kiondo, tumempeleka Ruvu Shooting. Kwanza kabisa ikumbukwe ni mchezaji wa kikosi cha U-20, lakini yeye na Fahad Fuad tumewapandisha hadi kikosi cha kwanza, lakini Kiondo tumpeleka huko, Fuhad bado yupo anasubiri timu yoyote ile ambayo itamhitaji," alisema Bumbuli.

Mchezaji huyo anayecheza nafasi ya ushambuliaji, ni wa pili kutolewa kwa mkopo kipindi hiki cha dirisha dogo, baada ya Juma Mahadhi kupelekwa Ihefu FC kwa mkopo na mechi yake ya kwanza ilikuwa dhidi ya timu yake hiyo hiyo, iliyochezwa Desemba 23, mwaka jana kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, Yanga ikishinda mabao 3-0.

# Kocha Mlandege aachia ngazi rasmi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Mlandege, Abdulmutik Haji, ameachana na timu hiyo ya Ligi Kuu Zanzibar, ikiwa ni miezi miwili tangu abebe jukumu hilo la kuinoa.

Mlandege inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama tano baada ya michezo minane ya Ligi Kuu Zanzibar ambayo kwa sasa imesimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi.


Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema wakati anaichukua timu hiyo hawakuwa na makubaliano ya kuwa kocha wa kudumu na kwamba, walichokubaliana ni kuifundisha katika kipindi ambacho timu hiyo ilikuwa ikikabiliwa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo tayari imetolewa baada ya kupoteza mechi zote mbili, nyumbani na ugenini.

"Nilikuwa kocha wa muda pale Mlandege na makubaliano yetu ilikuwa kwa ajili ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo niliendelea kusalia pale kwa kuwa uongozi wa timu hiyo ulikuwa upo mbioni kutafuta mwalimu ambaye atainoa timu hiyo kwa msimu huu," alisema.

# Michezo

Jumatano Januari 6, 2021

Nipashe

RAMOS SASA HURU KUONDOKA MADRID HABARI UK 22

NJOONI LEO MUONE...




Wachezaji wa Simba, beki Ibrahim Ame na kiungo Clatous Chama (kulia), wakiwa mazoezini, leo timu hiyo itaikaribisha FC Platinum ya Zimbabwe katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kwenye mechi ya marudiano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: MAKTBA YETU**

# SIMBA: NI USHINDI TU

## ●●●Platinum nao watamba wanajua pakuwashika kwa bao la ugenini, lakini waambiwa...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Tanzania Bara na wawakilishi wa nchini kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wamesema iwe jua ama mvua kazi yao ni moja tu watakapoikaribisha FC Platinum ya Zimbabwe leo, kuibuka na ushindi mzito na kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri mkubwa barani humu kwa ngazi ya klabu.

Simba imewaita mashabiki wote na Watanzania wanaiombea mema kufika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuishangilia mwanzo mwisho, wakiimba "WIDA, WIDA, WIDA (War in Dar)...", kaulimbiu ambayo wanaamini itakuwa ni hamasa kubwa kwa wachezaji wao dimbani kuibuka na ushindi.

Simba ambayo inahitaji ushindi wowote kuanzia mabao 2-0, ili kutinga hatua ya makundi kutokana na kupoteza mchezo wa awali kwa bao 1-0 ugenini nchini Zimbabwe, tayari Kocha Mkuu wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Sven Vandenbroeck, amesema jeshi lake lipo tayari kuibuka na ushindi na kilichobaki ni mashabiki kujitokeza kwa wingi kuipa sapoti timu hiyo.

"Tupo katika nafasi nzuri ya kushinda mechi hii ya marudiano kwa sababu wapinzani wetu si wakutisha," alisema.

"Hatukupoteza mechi ya kwanza ugenini kwa sababu ya ubora wao, bali tulipoteza kwa sababu ya makosa yetu."

"Waliweza kufunga na sasa tunapaswa kuwa makini tutakaporudiana."

Lakini Kocha wa FC Platinum, Norman Mapeza, amesema wapo hapa nchini kwa ajili ya kumalizia kazi waliyoianza Zimbabwe wiki mbili zilizopita, baada ya kuizamisha Simba katika dakika ya 17, shukrani zikimwendea Perfect Chikwende alijaza mpira kimyani.

"Tumekuja kufanya kazi ile ile na tupo tayari kupata ushindi na kufuzu hatua ya makundi, hakuna kingine, tunachofahamu wapinzani wetu wamejiandaa kisaikolojia na tunajua ni timu ngumu ikiwa nyumbani, tunaiheshimu, lakini hatuwaogopi.

"Tulipata ushindi wa bao 1-0 nyumbani, tulipaswa kufunga zaidi lakini wao pia, tunafaida kidogo tutahakikisha tunafunga mabao ya ugenini, tutawavuta na kadri watakavyokuja tutakuwa na nafasi ya kuwamaliza kwa mashambulizi ya kushtukiza."

Alipoulizwa ni mfumo gani watakaocheza dhidi ya Simba, Mapeza alisema: "Usijali, tunajua namna ya kushughulika nao, nimekuwa nikifuatilia mechi zao na ninajua namna ya kuwashika, utakuwa mchezo mzuri na lengo letu kuu ni kutinga hatua ya makundi."

Lakini kwa upande wa uongozi wa Simba, umesema kuwa kila kitu kimekamilika na mgeni rasmi katika mechi ya leo atakuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Damas Ndumbaro.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, amewataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kununua tiketi kwa wingi ambazo kwa VIP A ni Sh. 40,000, Platinum Sh. 150,000, VIP B na C ni Sh. 30,000 huku mzunguko akisema ni Sh. 7,000, ili kwenda kuishuhudia Simba ikiendeleza rekodi yake nzuri ya kutopoteza nyumbani kwenye mechi za kimataifa.

## `NAMUNGO YATINGA RAUNDI YA PILI CAF

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Namungo FC, wametinga raundi ya pili ya michuano hiyo kwa kuiondosha timu ya Al Hilal Obeid kwa jumla ya mabao 5-3 baada ya jana kulazimisha sare ya 3-3 ugenini katika mechi ya marudiano iliyopigwa Uwanja wa Al Hilal Omdurman mjini Khatoum, Sudan.

Namungo inaingia kwenye hatua hiyo, baada ya ushindi wa mabao 2-0 iliyoupata wiki mbili zilizopita hapa nchini kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Kwa matokeo hayo, Namungo itasubiri kucheza na moja kati ya timu zitakazotolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyoanza kuchezwa jana na mechi zingine zikichezwa leo na kama itaitoa basi itatinga moja kwa moja hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Namungo ilianza kuwashtukiza wageni dakika ya pili tu ya mchezo kwa bao lililofungwa na straika hatari raia wa Ghana, Steven Sey, lakini Al Hilal Obeid ilisawazisha dakika ya chache baadaye kupitia kwa Amin Ibrahim El Man.

Dakika ya 13, wenyeji waliandika bao la pili lililofungwa na Ibrahim Mohamed Ali, kabla ya kupata la tatu dakika tano baadaye likifungwa na Anwar Saadat.

Kuona hivyo, Namungo ilimtoa kipa Jonathan Nahimana na kumwingiza Nurdin Balora. Ilikuwa ni dakika ya 39, wakati Blaise Bigirimana alipoiandikia Namungo bao la pili, akiruka juu kuunganisha mpira wa krosi kutoka kwa Sixtus Sabilo na hadi mapumziko, wenyeji walikuwa mbele kwa mabao 3-2.

Dakika nne tu baada ya mapumziko, Namungo ilifanikiwa kusawazisha bao lililofungwa na beki wa kushoto, Edward Manyama kwa kichwa, kufuatia kizaazaa cha kona.

Kwenye michuano ya awali, Namungo FC iliitoa Al Rabita ya Sudan Kusini kwa jumla ya mabao 3-0, mechi ya kwanza ikishinda mabao hayo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam, na ikasonga mbele bila kurudiana kutokana na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kuifuta mechi hiyo ya marudiano baada ya Chama cha Soka cha Sudan kushindwa kugharamia safari za waamuzi ambao walitakiwa kwenda kuchezesha mechi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002